MATATIZO YA TAFSIRI NA UFASIRI KATIKA MAHAKAMA ZA KENYA: MFANO WA MAHAKAMA YA SHERIA YA KITALE

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

MWANGI WAIGANJO SAMMY

EGERTON UNIV ACQUISITIONS BOOK P.O. BOX 536 EGERTON 19 SEP 2013 LIBRARY

Ripoti hii imewasilishwa katika Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu, ili kutimiza baadhi ya mahitaji ya Shahada ya Uzamili katika Kiswahili ya Chuo Kikuu cha Egerton

CHUO KIKUU CHA EGERTON

DESEMBA, 2012

2013/96626

EULIB 041 008

UNGAMO NA IDHINI

UNGAMO

Ripoti hii ni kazi yangu asilia na haijawasilishwa katika chuo chochote kile kwa mahitaji ya shahada yoyote.

Mwangi Waiganjo Sammy

AM 12/1934/07

Sahihi _____

Tarehe 05-12-2012

IDHINI

Ripoti hii imewasilishwa kutahiniwa katika Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu kwa idhini yetu kama wasimamizi walioteuliwa rasmi na Chuo Kikuu cha Egerton.

PROF. Kitetu Catherine

Sahihi _____

Tarehe 05-12-2012

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu Chuo Kikuu cha Egerton

DR. Furaha Chai

Sahihi _____

Tarehe 05-12-2012

Idara ya Fasihi, Lugha na Isimu Chuo Kikuu cha Egerton

HATILINZI

Haki zote zimehifadhiwa. Hairuhusiwi kuiga, kunakili, kupigisha chapa, kutafsiri au kukitoa kitabu hiki kwa jinsi yoyote bila idhini ya mwandishi au chuo cha Egerton.

© Sammy W. Mwangi, 2012

TABARUKU

Naitabaruku ripoti hii kwa wapendwa wafuatao: Kwa wavyele wangu Isaac Mwangi, Grace Njoki na Beatrice Thuguri. Mke wangu mpendwa Shelmith pamoja na watoto wangu: Grace, Jim, Isaac na Betty kezzy.

SHUKRANI

Namshukuru Rabuka kwa kunipa ari na moyo wa kusoma kwa kina. Shukrani zangu za dhati nazitoa kwa wasimamizi wangu Prof. Kitetu Catherine na Dr. Furaha Chai. Prof. Kitetu alinifunza mbinu za utafiti zilizonifaa si haba, himizo lake wakati moyo wangu ulikuwa umebondeka lilikuwa dawa kwangu. Dr. Chai wewe ni wa kuigwa ulinifunza mengi kuhusu lugha na utamaduni. Sitasahau wosia wako kuwa licha ya changamoto zote, lazima "mtoto azaliwe". Shukrani za dhati kwa Dr. Beja ambaye alinikumbusha machungu ya masomo huja kwa muda mfupi lakini matunda yake hufurahiwa kwa muda mrefu. Mchango wako katika kozi ya tafsiri ilinifaa pakubwa. Shukrani tele kwa Dr. Mukuthuria na Prof. Onyango ambao walinifunza.

Shukrani kwa wenzangu Nkanatha Johnson na Cecilia Gekonga tuliotia makali pamoja kwa kujivunia na kutukuza lugha ya Kiswahili. Isitoshe, wanafunzi wa uzamili 2007 wa Lugha: Bichang'a Nyaigoti, Rachel Nyambura, Joyce Boke, Norah Atambo, na mwendazake Linnah Cheres. Pia, marafiki wa dhati Jared, lynette, Kwambai na Bosire nawashukuru kwa msaada wenu.

Nampongeza jaji mkuu wa Mahakama ya Kitale kwa msaada mkubwa wakati wa utafiti. Pia wakili Ann Kibe, Bw. Kibe na Bi. Winnie Bett nawashukuru kwa kunielekeza.

Shukrani kwa tume ya kuwaajiri waalimu pamoja na mwalimu mkuu wa shule ya upili ya St. Antony's Kitale, Bw. Nabungolo kwa kunipa kibali cha miaka miwili kujiendeleza kitaaluma. Isitoshe, mkuu wa shule ya upili Uasin Gishu Bw. Kogo kwa kuniwezesha kuandaa ripoti yangu bila bugudha.

Naienzi familia yangu kwa uvumilivu mkubwa wakati wa kipindi hiki cha kusoma. Shukrani tele kwa mke mpendwa Shelmith kwa dua zako kwa maulana, kuwalea wanetu katika kipindi hicho na himizo la kila mara nisome kwa bidii. Kwa wenetu: Grace, Jim, Isaac na Kezzy, mlikuwa himizo kwangu nitie bidii za mchwa.

Tamati, shukrani zangu ziwaendee wote waliochangia kazi hii kwa njia moja au nyingine lakini labda nikasahau kuwatambua.

IKISIRI

Lugha ya Kiingereza hutumika kama lugha rasmi ya mahakama nchini Kenya. Hata hivyo kwa sababu ya wingi lugha, ukalimani hufanywa ili kuwawezesha wale ambao hawaelewi Kiingereza kuelewana kupitia mkalimani. Nia ya ukalimani ni kuwezesha mawasiliano kutoka lugha moja hadi nyingine. Mkalimani hutekeleza jukumu muhimu katika mchakato huu wa uchanganuzi ili kupitisha ujumbe ipasavyo. Hata hivyo, sehemu ya ujumbe hupotea au waweza kubadilishwa ukalimani unapofanywa. Jambo hili litafanya maamuzi au hukumu inayotolewa isieleweke vyema kwa mlalamishi au mshtakiwa hivyo, kukiuka haki za kibinadamu. Utafiti huu ulitambulisha na kueleza matatizo ya tafsiri na ufasiri na pia, kubainisha chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri. Nadharia tete za utafiti huu zilikuwa ni kwamba kuna matatizo mengi ya tafsiri na ufasiri katika mahakama ambayo yana chanzo. Utafiti huu uliongozwa na nadharia ya tafsiri ya Nida inayosema kuwa tafsiri ni sheria ama utaratibu ambao mfasiri anahitajika kuufuata ili kupata ujumbe uliokusudiwa kutoka kwa lugha chanzi hadi lugha lengwa. Ukalimani ulifanywa kutoka lugha ya Kiingereza hadi Kiswahili. Deta iliyokusanywa ilikuwa ni matamko yaliyofasiriwa katika shughuli za mahakama baina ya mshtaki na mshtakiwa kwa kunakili vikao 9 vya mahojiano. Isitoshe, wasailiwa 9 waliofanya ukalimani pamoja na hadhira ya watu 9 walichaguliwa kimakusudi na kuhojiwa juu ya matamko ya ukalimani ili kuchangia deta ambayo ilinukuliwa. Deta ilichanganuliwa kimaelezo ili kufikia hatima mwafaka. Utafiti ulibainisha kuwa kulikuwa na matatizo mbalimbali katika shughuli za mahakama yaliyofasiriwa. Matatizo yaliyotambuliwa ni ya udondoshaji, nyongeza, matatizo ya kiutamaduni na ujumbe uliopotoka. Matatizo haya yalitokana na kuwa wakalimani hawakutekeleza wajibu wao ipasavyo kwa kutozingatia maadili ya kazi yao. Mtafiti anapendekeza kuwa kuna haja ya kuwapa wakalimani mafunzo katika tafsiri na ufasiri ili kuinua kiwango cha ujuzi na ufahamu wa majukumu yao. Matokeo ya utafiti huu yatachangia usomi wa kiisimu hasa isimu–jamii na somo la tafsiri na ufasiri. Pia, yatakuwa ya manufaa kwa wasomi na taasisi ya sheria.

ABSTRACT

English is used as the official language of the court in Kenya. However, in a multilingual setting where contact between different linguistic communities is unavoidable, interpretation services are provided for those who do not understand English. The interpreter is supposed to bridge the linguistic divide. The purpose of interpretation is normally to communicate the intended information from one language to another. The process of interpretation, however, involves not only linguistic factors, but also extra-linguistic parameters whereby 'message bits' are lost or the whole message may be distorted. Such alterations may have an impact on the legal messages to the complainant or the defendant, leading them not to understand the ultimate judgments hence violating their human rights. The study identified and described interpretation and translation problems in the court. The origin of interpreter errors were also described. The study was based on the hypothesis that there were interpretation and translations problems in courts and these errors had an origin. The study was guided by Nida's theory of translation which says translation is a scientific process that requires one to preserve intended information from source language to target language. Data was collected by tape-recording nine court interviews from the complainant and the defendant where interpretation was done. Identified Interpreted utterances from the complainant and the defendant formed the data. In addition, nine court clerks who are interpreters and nine persons forming the court audience were selected purposively and interviewed regarding the interpreted utterances to supplement on the data that was transcribed. The data elicited was analysed qualitatively to arrive at inferences and conclusions. The study revealed that there were various interpreter errors in the interpreted proceedings that included omissions, additions, cultural barriers and distortion. The errors arose from the fact that the interpreters failed to understand their defined roles and procedure of ethics. There is a need to train them courses in court translation and interpretation for effective skills, competence in language and their role as court interpreters in the administration of justice. The study findings would contribute to the study of linguistics specifically in the area of socio-linguistics in translations and interpretation. The study is useful to the Law institutions and academicians.

ASFER TON ... IBRARY

YALIYOMO

UNGAMO NA IDHINI ii
HATILINZI iii
TABARUKU iv
SHUKRANI v
IKISIRI vi
ABSTRACT vii
YALIYOMO viii
ORODHA YA JEDWALI xi
VIFUPISHO xii
SURA YA KWANZA: UTANGULIZI 1
1.1 Usuli wa mada 1
1.2 Mada ya utafiti 4
1.3 Madhumuni ya utafiti 4
1.4 Nadharia tete 4
1.5 Umuhimu wa utafiti 4
1.6 Upeo wa utafiti 5
1.7 Ufafanuzi wa istilahi 6
SURA YA PILI: MAPITIO YA MAANDIKO NA MSINGI WA NADHARIA 7
2. 1 Utangulizi 7
2.2 Tafiti mbalimbali katika tafsiri na ufasiri 7
2.2.1 Lugha na utamaduni 7
2.2.2 Wajibu / majukumu ya mfasiri katika Mchakato wa ufasiri 10
2.3 Msingi wa nadharia ya tafsiri ya Nida 13
SURA YA TATU: MBINU ZA UTAFITI 17
3.1 Utangulizi 17
3.2 Muundo wa utafiti 17
3.3 Eneo la utafiti 17
3.4 Uteuzi wa sampuli 18
3.5 Ukusanyaji deta 18

3. 5.1 Mahojiano 18
3.5.2 Uchanganuzi wa matamko yaliyorekodiwa 19
3.6 Uchanganuzi wa deta 20
SURA YA NNE: UWASILISHAJI, UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA 22
4.1 Utangulizi 22
4.2 Maoni ya wakalimani kuhusu ukalimani kutokana na Mahojiano 22
4.2.1 Taarifa za kimsingi 22
4.2.2 Jinsia ya wakalimani 22
4.2.3 Umri wa wakalimani 23
4.2.4 Elimu ya wakalimani 23
4.2.5 Tajriba katika ukalimani 24
4.2.6 Kozi za ukalimani 25
4.2.7 Maoni ya wakalimani kuhusu mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani ... 26
4.2.8 Maoni kuhusu ufahamu wa wajibu / majukumu ya mkalimani 26
4.2.9 Maoni kuhusu matayarisho wanayofanya kabla ya ukalimani 27
4.2.10 Maoni ya washtakiwa / washtaki kuhusu ukalimani 28
4.2.11 Maoni kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wakalimani 28
4.2.12 Maoni jinsi ya kukabiliana na matatizo 29
4.3 Maoni kuhusu tafsiri ya istilahi mbalimbali 29
4.3.1. Mitigation 30
4.3.2 Defense 30
4.3.3 Carnal knowledge 31
4.3.4 Plea 31
4. 3.5 Burglary and housebreaking 31
4.3.6 Jurisdiction 32
4.3.7 Cross-examination 32
4. 3.8 Robbery with violence 32
4.3.9 Confessions 33
4.3.10 Indecent assault 33
4.4 Maoni ya hadhira kuhusu tafsiri 34

4.4.1 Maoni ya hadhira jinsi ukalimani ulivyofanywa 34
4.4.2 Maoni ya hadhira kuhusu maamuzi yanayofanywa na hakimu 36
4.4.3 Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikutafsiriwa vizuri 36
4.4.4 Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikueleweka 37
4.5 Uchanganuzi wa matamko yaliyokalimaniwa 37
4.5.1 Muhtasari wa matamko yaliyonaswa, tarehe, saa, nambari ya kesi na ilihusu nini 38
4.6 Maelezo ya matatizo ya tafsiri na ufasiri 38
4.6.1 Makosa yatokanayo na utamaduni 39
4.6.3 Makosa ya nyongeza 45
4.6.4 Maana potovu 47
4.6.5 Makosa anuwai 48
4.7 Kubainisha kiini / chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri 49
4.7.1 Ufahamu wa majukumu/ wajibu wa mkalimani 49
SURA YA TANO: MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO 54
5.1 Utangulizi 54
5.2 Muhtasari wa matokeo 54
5.2.1 Kutambulisha na kueleza matatizo ya tafsiri na ufasiri 54
5.2.2 Kubainisha kiini / chanzo mbalimbali ya matatizo ya tafsiri na ufasiri 56
5.3 Hitimisho 56
5.3 Mchango wa utafiti 57
5.4 Matatizo yaliyomkabili Mtafiti 57
5.5 Mapendekezo 57
5.6 Utafiti zaidi 59
MAREJELEO 60
KIAMBATISHO A 65
KIAMBATISHO B 68
KIAMBATISHO C 69

ORODHA YA JEDWALI

Jedwali 1 : Jinsia ya wakalimani..... 22

Jedwali 2 : Umri wa wakalimani..... 23

Jedwali 3 : Elimu ya wakalimani..... 23

Jedwali 4 : Tajriba katika ukalimani 24

Jedwali 5 : Kozi za ukalimani 25

Jedwali 6 : Maoni kuhusu mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani..... 26

Jedwali 7 : Maoni kuhusu ufahamu wa majukumu / wajibu wa mkalimani 27

Jedwali 8 : Maoni kuhusu matayarisho wanayofanya kabla ya ukalimani 27

Jedwali 9 : Maoni kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wakalimani 28

Jedwali 10 : Maoni ya tafsiri ya istilahi mbalimbali 29

Jedwali 11 : Maoni ya hadhira jinsi ukalimani ulivyofanywa 35

Jedwali 12 : Maoni ya hadhira kuhusu maamuzi yanayofanywa na hakimu 36

Jedwali 13 : Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikutafsiriwa vizuri 36

Jedwali 14 : Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikueleweka 37

Jedwali 15 : Muhtasari wa matamko yaliyonaswa, tarehe, saa, nambari ya kesi 38

Jedwali 16 : Matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama ya Kitale 39

Jedwali 17 : Muhtasari wa matamko kuhusu ufahamu wa wajibu wa mkalimani.....49

VIFUPISHO

LC : Lugha chanzi. Hii ni lugha asilia

LL : Lugha lengwa. Hii ni lugha pokezi.

SURA YA KWANZA
UTANGULIZI

Sura hii inatuelezea usuli wa mada kwa kuangazia ukalimani katika sehemu mbalimbali ulimwenguni. Isitoshe, tumeangazia matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama ya Kitale. Vilevile, tumejadili, mada ya utafiti, madhumuni ya utafiti, nadharia tete, umuhimu wa utafiti, upeo wa utafiti na ufafanuzi wa istilahi.

1.1 Usuli wa mada

Ufasiri wa aina yoyote ni lazima uongozwe na uzingativu wa uhakika na ukweli wa ujumbe uliomo mbali na kutambua upekee wa lugha na utamaduni ambapo tafsiri inatumika. Tamko lolote lile lina nia ya kimawasiliano na mawasiliano lazima yajumuishe pande mbili kama ilivyo katika lugha chanzi (LC) na lugha lengwa (LL).

Nchi ya Ireland iliathirika zaidi kwa sababu ya kuwa na makabila na lahaja zaidi ya mia mbili kutokana na wakimbizi waliohamia huko au wafanyi kazi kutoka sehemu mbalimbali. Kiairishi na Kiingereza ndicho kilitambulika na kutumika zaidi hivyo basi wakalimani wengi walihitajika kuzimudu lugha hizi. Mashirika ya kibinafsi ndiyo yaliyochukua wajibu huu wa kuwafunza wakalimani ili kukidhi mahitaji ya jamii. Licha ya kazi ya mashirika haya, ubora wa ukalimani umeendelea kudhoofika. Inaaminika kuwa iwapo unaweza kuzielewa na kuziongea lugha mbili basi unafuzu kuwa mkalimani. Jambo ambalo (Gonzalez, 1991) anasema ni hatari kwa kuwa mkalimani wa mahakama anahitaji kukalimani au kuhamisha ujumbe au habari kutoka LC hadi LL bila kufupisha wala kuongeza huku akihifadhi mtindo na muundo wa lugha huku akizingatia lengo la mwandishi. Gonzalez anatoa nchi ya Uholanzi kama taifa ambalo wakalimani hujifunza barabara sawa na nchi ya Uingereza.

Mazrui (1998) anabainisha kuwa Tanzania na Kenya ni mataifa ambayo yamefanikiwa kukuza lugha ya Kiswahili hasa bungeni ingawa bado Kiswahili hakijapewa hadhi katika maswala ya kisheria.

Mutunga (1990) anabainisha kuwa Katika mataifa mengi ya Kiafrika, Kiingereza ndicho lugha rasmi ya kisheria katika shughuli za mahakama. Katiba Ya Kenya (2010) katika kifungu 50 (m) inasema,

> *Every accused person has the right to a fair trial which includes the right to have the assistance of an interpreter without payment if the accused person cannot understand*

the language used at the trial

Mshtakiwa ana haki ya kutumia lugha anayoielewa kwa kutumia usaidizi wa mfasiri bila malipo yoyote. Hata hivyo watu wengi walio na kesi hasa katika sehemu za mashambani hawaelewi Kiingereza vizuri na hata uelewa wao wa Kiswahili ni wa kiasi fulani. Ukalimani unakuwa ni muhimu sana kwa sababu wale ambao hawajimudu katika Kiingereza inabidi wafasiriwe hadi lugha wanazozielewa.

Mazrui (1998) ameainisha sifa za mkalimani bora:

1. Mkalimani stadi ni yule aliye na ujuzi wa lugha zote mbili; lugha chanzi na lugha lengwa.
2. Ana maarifa ya masuala ya sajili ya kortini na masuala ya sheria za lugha zote mbili.
3. Ana umilisi wa lugha zote mbili kiasi kwamba anaelewa tofauti za kiisimu katika lugha hizo na kuzingatia vibadiliki kama uana, umri na vipengele vya mazingira.
4. Anaelewa tamaduni za lugha chanzi na lugha lengwa

Mutunga (1990) anabainisha kuwa ukalimani unapofanywa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili kumbukumbu za ushahidi huandikwa kwa Kiingereza. Matokeo ya ushahidi ni kukosa usahihi, kutoeleweka vizuri, mchaganyiko wa masuala pamoja na makosa mengi ya sarufi. Usahihi wa ushahidi ni msingi wa utoaji haki. Wakati wa rufani mahakama kuu hutegemea kumbukumbu za mahakama ya wilaya ambazo hudhaniwa kuwa sahihi. Kumbukumbu zinapokuwa sio sahihi au kutoeleweka vyema husababisha matatizo makubwa na wakati mwingine haki kutotendeka.

Sure (1991) amebainisha mahusiano yalikuwepo baina ya makundi ya kijamii ya Kenya katika miaka 200 iliyopita.Watu walielewana kwa kuwa na lugha moja, mila sawa na hali za kijamii na kisiasa walizoelewa. Haya yalifanya wenyeji kuheshimu maadili ya jamii zao. Mizozo ilipozuka baraza la wazee lilitatua shida hizi. Utawala wa Kikoloni na Kiingereza uliharibu kanuni hizi. Kulitokea makundi yao kutegemea lugha, dini, mila za kwao, kundi la kitabaka huku kukiwa na ubaguzi wa rangi vilevile. Makundi haya yote yalihitajika kuwa na lugha unganishi. Sure anadai kuwa hii ilibidi kuwa na matumizi ya lazima ya lugha fulani iwe rasmi au ya kitaifa. Isitoshe, kwa kutumia lugha hizi hasa Kiingereza kulikuwa na matatizo mengi hasa katika mahakama hasa pale ambapo mshtaki hakuelewa Kiingereza. Katika hali hii ukalimani ulihitajika. Tatizo lilitokea kwa sababu ya utata katika lugha ya kisheria.

Sheria za Kenya zilizoandikwa zimetokana na manukuu ya vitabu vya sheria za Kiingereza zilizoathirika kwa istilahi na msamiati wa Kifaransa, Kilatini, na Kigiriki. Sajili ya sheria za

mahakama ni lugha ya kisheria katika kiwango maalum cha matumizi mahakamani. Huu ni mtindo wa lugha kulingana na hali za kisheria. Sajili huakisi umilisi wa kimawasilano wa msemaji anayetazamiwa kuteua msamiati wa matini kutoka faridi iliyoko kulingana na mahitaji ya mktadha huo. Kwa hivyo, sajili ya sheria za mahakama ni uwezekano wa Kisemantiki ambao unaamuliwa na utamaduni wa jamii ambapo ruwaza za mazingira hayo hutokea. Mazingira ya mahakama kwa upande wake ni muktadha ambao huamua na kuamuliwa kwa matumizi ya lugha maalum. Lugha ya mahakama hutudokezea uhusiano unaorudiwarudiwa kati ya sifa za muktadha wa mahakama na lugha inayotumika humo. Hali hii ndiyo hufanya urasmi wa lugha inayotumika mahakamani kuwa tofauti na matumizi ya lugha katika miktadha mengineyo.

Utafiti huu ulifanywa katika mahakama ya sheria ya Kitale. Mji wa Kitale ndio mji mkuu katika kaunti ya Trans-Nzoia. Mahakama ya Kitale ilichaguliwa kwa sababu ya umuhimu wake kihistoria ambapo rais wa kwanza nchini Kenya hayati mzee Jomo Kenyatta pamoja na mashujaa wa kisiasa walipokuwa gerezani kule Kapenguria kesi yao ilikuwa ikifanywa katika mahakama hii. Pia, hili ni eneo la ukulima na kuna kesi nyingi za mashamba, wizi, visa vya uvunjaji sheria wa barabara unaofanywa na waendeshaji wa magari, pikipiki au baiskeli. Isitoshe, mahakama ya Kitale inahudumia eneo kubwa ikiwa ni pamoja na jamii wanaohamahama kwa kutafuta malisho ya mifugo. Ukalimani unatumika sana kwa sababu ya hoja za kijamii baadhi ya wahusika hawana kisomo.

Kulingana na takwimu za mahakama za Kitale kulikuwa na kesi za madai 5089 na za jinai 6481 ambazo zilikuwa mahakamani zikisubiri kusikizwa. Katika kesi hizi za jinai ukalimani ulitumika zaidi kwa sababu ni bora mshtakiwa angeelezwa kile kinachoendelea kabla uamuzi wa jaji kutolewa. Wengi wa wahalifu huwa na changamoto za kimasomo au fedha za kupata wakili. Kumekuwa na malalamishi mengi katika mahakama ya sheria ya Kitale hasa katika kesi ambapo ukalimani umefanywa ambapo mshtakiwa hahusishwi ipasavyo katika lugha anayoijua vyema. Matatizo haya ni kutokana na tafsiri na ufasiri unaofanywa na mfasiri huku ukichukuliwa kuwa ni sahihi.

Human Rights Watch (2010) katika mahakama ya Kitale inabainisha kuwa washukiwa wa kikundi kutoka jamii ya Wasabaot lililozozania shamba katika eneo la mlima Elgon washtakiwa wengi hawakuelewa maamuzi yaliyotolewa kortini kutokana na ukalimani hivyo waliomba Mahakama ya Kimataifa ya Haki za Binadamu kuchunguza haki za kujieleza. Juhudi zimechukuliwa na mahakama kwa kujaribu kuajiri makarani kutoka jamii mbalimbali

wakizingatia kuwa mfasiri aelewe lugha ya Kiswahili, Kiingereza na lugha ya asili yoyote ile ili kukiwa na haja ya ufasiri watekeleze huduma hii. Licha ya juhudi hizi bado kuna malalamishi.

Licha ya ulalamishi na kesi nyingi za rufaa zinazotokana na ukalimani potovu utafiti wa kiakademia haujafanywa katika mahakama ya sheria ya Kitale ili kutambua matatizo ya tafsiri na ufasiri na pia kubainisha chanzo cha matatizo. Utafiti huu ulichunguza jinsi tafsiri na ufasiri hufanywa katika shughuli za mahakama.

1.2 Mada ya utafiti

Licha ya umuhimu wa ukalimani mahakamani, mshtakiwa hunyimwa haki yake ambapo hauhusishwi ipasavyo katika shughuli za mahakama na pale ambapo ukalimani hufanywa na sehemu zingine kuachwa au kuongezwa. Isitoshe, ukalimani husababisha ujumbe ambao umepotoka hivyo kumfanya mshtaki / mshtakiwa kukosa kuelewa uamuzi unaotolewa na hakimu swala linalokiuka haki za binadamu za kujieleza. Utafiti huu ulinuia kutambulisha matatizo ya tafsiri na ufasiri mahakamani.

1.3 Madhumuni ya utafiti

Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni:

i. Kutambulisha na kueleza matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama ya Kitale.
ii. Kubainisha kiini / chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama ya Kitale.

1.4 Nadharia tete

i. Kuna matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama za Kitale.
ii. Kuna kiini / chanzo mbalimbali ya matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama za Kitale.

1.5 Umuhimu wa utafiti

Utafiti huu utakuwa muhimu katika kuonyesha haja ya kufanikisha mawasiliano katika jamii. Wanaisimu wataweza kufaidika kutokana na ulinganishi utakaofanyiwa lugha zinazohusika katika kuelewa tofauti za kimiundo za lugha hizo. Kwa taasisi ya sheria, itawasaidia hasa wakalimani, wanasheria na wanaotoa sera kwa kuangazia baadhi ya matatizo yanayotokana na ukalimani na tafsiri. Utafiti huu utaweza kuongeza ujuzi katika ukalimani baada ya kubainisha

chanzo cha matatizo ya ukalimani na kupendekeza njia za kukabiliana nazo. Kwa wasomi ni eneo muhimu sana kwa sababu itapanua kuelewa masuala mengi ya sajili ya sheria kwa lugha ya Kiswahili; kutokana na kuwa kazi nyingi za mahakama ambazo zimetafitiwa au kuandikwa zimetumia Kiingereza.

Matokeo ya utafiti yatatumiwa kama msingi wa utafiti katika lugha zingine. Utafiti huu utakuwa wa manufaa kwa wafasiri, wahadhiri, au wataalamu mbalimbali wanaofanya utafiti katika ukalimani. Inatarajiwa kuwa ujuzi wao utaweza kuboreshwa na pia kutoa changamoto za kuwa na huduma kabambe za kuwafunza wakalimani ili kuboresha viwango vya ufasiri nchini.

Utafiti huu utatoa changamoto zaidi kwa watafiti kufanya utafiti zaidi katika lugha nyingine na utafiti katika ukalimani katika nyanja mbalimbali. Matokeo ya utafiti pia yatachangia katika taaluma ya sheria kwa kuangazia msingi bora katika kazi ya ufasiri mahakamani.

Utafiti huu pia, utapigania masuala ya kiisimu ambapo ni vyema mshtaki au mshtakiwa apewe haki ya kujieleza ipasvyo bila kufungwa na lugha yoyote ile. Ujumbe ulio katika lugha chanzi (LC) uwe sawa katika lugha lengwa (LL) bila kubadilisha maana ya matamko.

Ujuzi, maarifa na uwajibikaji wa mfasiri utaboresha zaidi ukalimani. Hii yaweza kupatikana kupitia mafunzo maalumu katika tafsiri na ufasiri. Hii ni kwa kupitia kozi ambazo zitapangwa kwa utaratibu maalumu zikiangazia chanzo cha matatizo ya ukalimani, matatizo mbalimbali, utamaduni na lugha.

1.6 Upeo wa utafiti

Utafiti huu ulijikita katika kesi za jinai ambazo zilikuwa na ukalimani katika mahakama ya Kitale zilizohusisha washtakiwa na walalamishi. Mtafiti alishughulikia matatizo ya ukalimani kutoka kwa tunukuzi za ukalimani uliofanywa kutoka Kiingereza hadi Kiswahili. Ingawa kulikuwa na ukalimani wa lugha nyingine za makabila mbalimbali utafiti huu haukuzingatia hayo. Mtafiti alichanganua msamiati na Semantiki katika kutambua matatizo katika ukalimani. Lugha ya Kiswahili ilichaguliwa kwa sababu ni lugha ya taifa na rasmi ilhali Kiingereza ni lugha rasmi nchini Kenya.

1.7 Ufafanuzi wa istilahi

Matamko	:	Usemi, matamshi au maneno. Haya ni yaliyokuwa yametafsiriwa na kunaswa.
Matatizo	:	Haya ni makosa, kasoro au udhaifu unaofanywa ambapo ujumbe ulio katika lugha chanzi huwa tofauti na lugha pokezi.
Mkalimani	:	Mtu anayehamisha habari iliyo katika lugha moja kwenda katika lugha nyingine kwa kusema.
Shughuli za mahakama	:	Majadiliano au mahojiano katika kesi.
Tafsiri	:	Kuhamisha habari kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kufuata Urasmi.
Tunukuzi	:	Habari iliotolewa katika matamshi na kuwekwa katika maandishi.
Ufasiri	:	Tendo la kuhamisha habari iliyo katika lugha nyingine kwa kusema. Katika muktadha huu neno hili limetumika kuhamisha ujumbe kutoka lugha chanzi hadi lugha lengwa.
Ukalimani	:	Kitendo cha kuhamisha habari kutoka lugha moja hadi nyingine kwa kusema.
Viziada lugha	:	Sifa za usemaji ambazo ni sehemu ya mfumo wa lugha. Viziada lugha huhusu matumizi ya mwili katika kuashiria, kuitikia, kukataa na kadhalika.

SURA YA PILI

MAPITIO YA MAANDIKO NA MSINGI WA NADHARIA

2. 1 Utangulizi

Sura hii inashughulikia mapitio ya maandiko ambayo yamegawanywa katika sehemu kulingana na mada huku tukizingatia madhumuni ya utafiti. Sehemu ya kwanza inaeleza utafiti mbalimbali katika tafsiri na ufasiri. Sehemu ya pili inatoa maelezo ya wataalamu mbalimbali kuhusu chanzo cha matatizo ya ufasiri na ufasiri kwa kujadili lugha na utamaduni. Pia wajibu / majukumu ya wafasiri yamejadiliwa katika kubainisha chanzo cha matatizo. Vilevile, nadharia ya tafsiri ya Nida inayoongoza utafiti huu imejadiliwa.

2.2 Tafiti mbalimbali katika tafsiri na ufasiri

Sehemu hii inaeleza utafiti mbalimbali kuhusu utamaduni na lugha. Lugha ni muhimu katika maelewano ya utamaduni. Kwa kuelewa utamaduni wa jamii mfasiri angeweza kuelewa jinsi anavyoweza kufasiri lugha. Vilevile, sehemu hii ilitoa maelezo kuhusu mkalimani kujua wajibu wake katika kufanya tafsiri na ufasiri. Tafiti hizi ziliweza kuonyesha michango yao au pengo tuliokuwa tukishughulika katika kutambua na kubainisha matatizo ya ufasiri na pia, kubainisha chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama.

2.2.1 Lugha na utamaduni

Danet (1980) alizingatia ethnografia ya mazungumzo na maana ya usemi. Mchango wa kuzielewa mila za mshukiwa ili kufanikisha mawasiliano mahakamana kutoa maamuzi ya haki kushughulikiwa. Washukiwa wa mila tofauti na zile za Kiafrika wanapotumia lugha ya Kiingereza, sheria za mila za kigeni haki haitekelezwe. Utafiti huu ni muhimu unaonyesha umuhimu wa kuelewa utamaduni na lugha mambo ambayo mtafiti alichunguza.

Loftus (1981) ameonyesha kuwa maumbo kauli ya kutendewa yanapotumiwa na maswali ya kuelekeza, mshukiwa hupotoshwa katika ushauri wake. Hii ni kwa sababu hana ujuzi wa lugha ya kisheria kumwezesha kujieleza vilivyo. Mara nyingi mshukiwa hujikuta taabani iwapo sehemu fulani itadondoshwa. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu tuliweza kutambua udondoshaji kama baadhi ya matatizo jambo ambalo tuliona ni udhaifu kwa upande wa mfasiri

Walker (1982) ameonyesha kuwa kukatizana katika maongezi husababisha vizuizi. Pia uelewano hutatizika mahali wanaohusika katika shughuli za mahakama hawatapewa fursa ya

kujieleza ipasavyo hivyo hadhira huondoka wakihisi haki haikutekelezwa. Hii ilitusaidia kwa sababu pale washtakiwa hawakupewa nafasi yao ilionekana mfasiri aliongeza ujumbe ambao haukukusudiwa . Utafiti huu basi ulitusaidia kuona jinsi nyongeza katika tafsiri inaweza leta matatizo, jambo tulilochunguza.

Newmark (1988) anadhihirisha kuwa utamaduni ni mkusanyiko wa mila na desturi zote za jamii inayotumia lugha moja mahsusi kama njia yake ya mawasiliano. Lugha basi ni kipengee na kielelezo cha utamaduni wa jamii. Msamiati wa lugha hujenga maana za maneno kutokana na utamaduni wa jamii inamozungumzwa lugha hiyo. Hivyo, maana za maneno ni kiungo au daraja madhubuti kati ya utamaduni na lugha na hicho ndicho kitovu cha ukalimani. Ukalimani siyo tu mchakato wa kiisimu bali pia ni mchakato unaojumuisha masuala yanayohusu utamaduni. Ili kufasiri dhana za kitamaduni mkalimani anawajibika kuelewa tamaduni za lugha zote mbili anazozishughulikia. Umahsusi wa lugha ni jambo tulilozingatia katika kuangalia matamko yaliyofasiriwa katika mahakama. Ukosefu wa uelewa huu uliweza kusababisha matatizo katika ujumbe wa LL.

Milroy (1987) ameonyesha jinsi ushahidi wa lugha ya maongezi ulivyo wa muhimu katika kutoa hukumu. Utumizi wake ulikuwa matumizi ya kanda ili kunasa sauti za mtu aliyedai arumbatwe. Huu ni utafiti wa mazingira ya kigeni na wetu. Utafiti huu ulituongoza kuona faida ya kumruhusu mshukiwa asikike mwenyewe mahakamani ikiwezekana awe na maongezi ya moja na hakimu ili kumpa nafasi ya kumkagua kisha akisia juu ya ukweli wake. Utafiti huu ni muhimu kwetu kwa sababu ulionyesha kuwa mtu hueleweka vyema akijieleza. Ni muhimu kutambua kuwa pia, tulitumia mbinu hii kama njia kukusanya deta kwa kurekodi matamko na kisha tukachanganua matatizo yaliyojitokeza.

Seligson (1990) anataja mambo ambayo yanahitaji kuzingatiwa ili kuwa na ukalimani mwema. Mkalimani ni vyema kuelewa sajili husika inayotumika kwa wakati huo, maana na athari ya tamko na utamaduni. Vigezo hivi visipozingatiwa hufanya ukalimani kuwa mgumu na iwapo vitazingatiwa vitafanikisha ukalimani. Katika utafiti wake wa mahakama za Kihispania za Amerika alitambua kwamba wakalimani wengi hawakuzingatia pragmatiki hivyo kupotosha maana iliokusudiwa. Kazi ya Mtaalamu huyo ilikuwa katika mazingira ya Kihispania. Katika utafiti wetu mazingira yalikuwa ya lugha ya Kiingereza na Kiswahili na tulichunguza matamko yaliyofasiriwa ili tuone maana zilizojitokeza.

Mwansoko (1996) anasema ili kufasiri matini zenye dhana za kitamaduni mfasiri anayetumia lugha za Kiingereza na Kiswahili huhitajika kupata "visawe vya kitamaduni" vilivyo mwafaka katika lugha anazozifanyia kazi. Visawe hivyo visipopatikana, basi mfasiri hupata matatizo makubwa. Kulingana na Nida (1964) visawe vinaweza kuainishwa katika makundi: ekolojia, violwa, mila na desturi, siasa na dini. Mkalimani anapokumbana navyo kisha akose visawe anaweza kuhamisha kwenye uzungumzi au LL ufafanuzi wa dhana hiyo inayohusika, anaweza kufanya ukopaji wa maneno, utohozi na kuchanganya ndimi. Nida anasema kwamba tofauti za kimazingira huleta matatizo katika kuyapata maneno yanayofanana au yanayowasilisha dhana moja. Kuna matatizo mengi yanayozuka tunaposhirikisha tamaduni mbili katika ukalimani. Baadhi ya matatizo ni: Kukalimani kijuujuu, kuyahepa baadhi ya maneno, kutopata uwiano halisi kwa sababu ya tofauti za kimazingira, utamaduni wa vifaa, wa kijamii, wa kidini na wa lugha. Utafiti huu ni muhimu kwani ulioana na madhumuni ya utafiti huu kwa kuangazia matatizo ya ufasiri na tafsiri kwa kuangalia lugha ya Kiingereza na Kiswahili. Hata hivyo, katika kazi yake ameangalia matatizo ya utamaduni katika kazi hii tulibainisha matatizo mengine yaliyochangia.

Mwansoko (1996) anabainisha tofauti za maumbo, miundo na maana kati ya Kiswahili na Kiingereza husababisha upungufu katika ukalimani. Maumbo ya Kiingereza kwa mfano, huruhusu kauli nyingi elekezi kutoonyesha umoja au wingi wa wahusika, wakati wala majina ya vitu mahsusi vinavyoambatana na maelekezo yanayotolewa. Hivyo mfumo huu wa maumbo huwezesha kutoa taarifa zilizopana zaidi. Kwa upande mwingine, mfumo wa Kiswahili hulazimu kubainisha vipengee vyote. Kwa mfano ili kufanikisha mawasiliano mtu anayekalimani kutoka lugha moja hadi nyingine wakati mwingine hulazimika kutumia kirai katika LL kuwasilisha dhana ambayo katika LC ni neno moja tu. Mfano "carnal knowledge" hatuna kisawe inakuwa "kuhusu mwili, tamaa za mwili". Hoja hizi za mwansoko ni muhimu katika kutoa mwanga kuhusu tofauti katika maumbo kati ya lugha mbili jambo ambalo hutatiza mawasiliano jambo tuliloshughulikia katika kazi hii. Hoja hizi ni muhimu zilichangia katika kuelewa umahsusi wa lugha hasa lugha ya sheria ambapo neno laweza kuwa na umahsusi kulingana na muktadha. Katika kazi hii mambo yaliyosababisha kuwa na utata katika mawasiliano tuliyachukulia kuwa ni 'matatizo'.

2.2.2 Wajibu / majukumu ya mfasiri katika Mchakato wa ufasiri

Mchakato wa ukalimani sio mwepesi kwa sababu ya hatua zinazofuatwa kutoka LC hadi LL hasa ikilinganishwa na tafsiri ambapo msomaji anaweza kusoma matini mara nyingi ili kuielewa kabla kuibuka na makala safi yaliotafsiriwa kutoka LC hadi LL. Katika ukalimani, mkalimani ni lazima aisikize habari kwa makini, afahamu vyema na kisha abadilishe ujumbe kutoka LC hadi LL mchakato unaostahili kuchukua sekunde chache. Mchakato wa ukalimani huchukua hatua 3: ufahamu, ubadalishaji ujumbe na uwasilishaji. Mchakato wa ukalimani huanza pale ambapo mkalimani ni vyema aelewe ujumbe ulio katika LC kama vile msemaji anavyokusudia. Akizungumzia suala hili (Thomas, 1983) anasisitiza iwapo msikilizaji hataelewa maana ya matamko yaliyokusudiwa na msemaji basi kutakuwa na vizuizi katika mawasiliano hata ingawa wasemaji watakuwa wakizungumza lugha ambayo kila mmoja anaelewa. Katika kuelewa ujumbe, unaweza kuathiriwa na ujuzi wa lugha, kiini cha habari au yale yanayojadiliwa, tamaduni za taasisi, utamaduni wa msemaji. Pia mkalimani huwa na tajriba kuhusu ulimwengu jambo linaloweza kuathiri jinsi atakavyoelewa ujumbe. Hoja hizi zilijikita katika yale yanayopitia akilini mwa mfasiri. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu ulionyesha kuwa chanzo cha matatizo ya ufasiri ni wale wanaofanya kazi hii. Hata hivyo, haikutoa ni kwa njia ipi mfasiri anahitajika kufanya kazi yake. Hili ndilo jambo tulilozingatia.

Mkalimani hufanya maamuzi ya fikra ni ipi njia bora ya kufanya ukalimani. Hufanya hivi kwa kutafuta visawe mwafaka katika LL. Mara nyingi ni vigumu kupata visawe vinavyolingana hivyo ni lazima afanye maamuzi ya kuchukua visawe ambavyo vitahifadhi ujumbe au kutoa maana na athari ya tamko sawa na ile ya LC kwa msikilizaji. Mkalimani anahitajika kuwa na ujuzi wa lugha, uwezo wa kukumbuka yaliyosemwa na pia awe msikilizaji mwema ili kufasiri ipasavyo ili uwasilishaji uwe bora (Wadensjö, 1990). Hoja hii ilikuwa muhimu kwetu ilitusaidia kuchunguza jinsi mfasiri alivyowasilisha mawazo yake. Hatua hizi ni muhimu katika kutambua aina za tafsiri alizochukua.

Biere (1978) ameonyesha kuwa kunahitajika mkalimani ambapo mshukiwa hana ujuzi wa lugha inayotumika mahakamani. Ametahadharisha kuwa mchango huo utatolewa na mkalimani mwenye elimu, ujuzi wa kutafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine. Mazingira tuliyofanyia utafiti huu yalionyesha kuwa mkalimani anahitajika kuwa na ufahamu wa ndani wa lugha zinazotumika.

Golingay (1995) alishughulikia mifano ya ufasiri wa maandiko matakatifu na kubaini kuwa wahubiri hamsini wanaweza kuzua mitazamo tofauti kuhusu matini moja. Aidha alieleza kuwa maana ya matini ya Biblia hupatikana kutoka kwa hadhira na kwamba matini moja inaweza kueleweka kwa njia mbalimbali na wasomaji mbalimbali. Utafiti huu ni muhimu kwa sababu maana ya tamko inaweza kufasiriwa kwa njia nyingi kulingana na vile mtu atakavyoelewa.

Kaschula (1995) anasisitiza kuwa wakalimani katika nyanja ya uanasheria ni lazima wawe waaminifu wanapofasiri ili kutoa tafsiri ya matamko ipasavyo. Anadai kuwa maneno ya sheria huwa na tafsiri maalum na maana inatakiwa izingatiwe. Umahsusi huu ndio tuliozingatia kwa kuchunguza umahsusi ulio katika Kiingereza. Umahsusi huu ndio tulionelea unakosa kuzingatiwa katika Kiswahili kwa sababu ya mahojiano ya kasi mahakamani. Mkalimani hufanya tafsiri ya moja kwa moja au fasiri za juujuu huku akiacha nje hoja zingine. Matokeo ni kupotea kwa ujumbe asili kwa kiasi kikubwa. Mkalimani hastahili kuegemea upande wowote. Vilevile hisia zake hazistahili kumwongoza katika ukalimani. Anawajibika asiegemee upande wa LC wala LL hivyo basi ni lazima afasiri ujumbe ipasavyo. Uchunguzi huu ni muhimu kwa sababu mtafiti alikuwa akitathmini uwajibikaji wa mkalimani.

Chimera na Nabea katika (Sunday Nation; August 3, 1997) wanasema lugha ndicho kipengele muhimu zaidi ya vyote katika mawasiliano na maelewano ya kitamaduni. Hapana yeyote anaweza kujiendeleza kufikia ufanisi kwa kutumia lugha asioweza kuimudu kikamilifu. Watu huweza kuyaeleza na kuyafafanua mambo ya msingi katika utamaduni wao kwa kutumia lugha wanayoimudu kikamilifu. Hii aghalabu huwa lugha yao ya kiasili. Maoni haya ya watafiti ni muhimu kwa sababu mtafiti alichunguza jinsi mawasiliano na maelewano hutekelezwa na wakalimani kortini.

Suala la wajibu wa mkalimani ni suala tata ambalo limeshughulikiwa na watalaamu mbalimbali huku wakichukua mielekeo tofauti (Gonzalez, 1991, Moeketsi, 1999, Roy, 2000). Kuna kundi la wakalimani wanaoamini kuwa wajibu wa mkalimani ni kuwasaidia wale ambao hawaelewi Kiingereza kuwafanikisha kushinda kesi. Hili ni jambo linalokiuka maadili ya kijamii na haki, kwa sababu wakalimani wa kitengo hiki hutoa ufafanuzi kinyume na jinsi ulivyo katika LC ili kuwawezesha wasioelewa Kiingereza kuelewa zaidi au wakati mwingine hufanya ukalimani unaowaelekeza kupata majibu jambo linalowafanya kushinda.

Kikundi cha pili ni kile ambacho kinaamini kuwa mkalimani hufanya kazi kama mashine. Kazi yake ni kurudia au kusema yale yanayosemwa kutoka lugha moja hadi nyingine. Msimamo

huu unashikiliwa sana na wanasheria ingawa wao huzingatia kuwa ni lazima ujuzi wa lugha utiliwe maanani. Kazi ya mkalimani ni kufanya ukalimani wa matamko jinsi yanavyowasilishwa bila kujali kama yanaeleweka au kama maana iliyokusudiwa imewasilishwa au la. Mawazo ya watalaam hao ilionyesha kuwa mfasiri huwa na lengo fulani anapofanya kazi yake. Hata hivyo, katika kazi zao hawaonyeshi athari za njia hizi jambo ambalo mtafiti alichunguza kama ndicho chanzo cha matatizo ya tafsri na ukalimani.

Wadensjö (1998) anashauri kuwa Mkalimani ana majukumu muhimu mbali na kufasiri anahitajika pia kuratibu. Mikkelson (1998) anasema kuwa licha ya wajibu huu muhimu walio nao wakalimani wengi hawauelewi kutokana na imani, mielekeo na mitazamo tofauti ya maisha inayoathiri ukalimani. Katika utafiti alioufanya alitambua kuwa lugha ya sheria ndio chanzo cha matatizo katika ukalimani wa Mahakamani kwa sababu jinsi inavyotumika inabidi kutafsiri neno kwa neno hasa ushahidi unapotolewa na hivyo kupotosha maana.Wazo hili ni muhimu kwa sababu mtafiti alichunguza njia au aina za tafsiri. Kila aina za tafsiri zina uzuri na udhaifu wake.

Okeiga (1998) alionyesha kuwa kutoelewana vilivyo katika muktadha wa mahakama za Kenya hutokana na matumizi ya sajili ya kisheria na kuwa wasaidizi wengi wa idara ya mahakama hawana maarifa ya kisheria. Isitoshe kwa sababu ya ugumu wa sheria ambazo zimeandikwa katika Kiingereza akapendekeza kuwa na kanuni za sajili ya kisheria katika lugha ya Kiswahili. Hoja hizi ni muhimu kwani ndizo tulizingatia katika kazi yetu. Katika kazi hii tuliangalia matatizo yaliyotinga mawasiliano na chanzo chake.

Roy (2000) anasema kuwa mkalimani anachukua wajibu wa wakili ilhali twajua hahitajiki kuegemea upande wowote. Mikkelson (2000) anasema kazi muhimu ya mkalimani ni kuhakikisha kuwa haki na usawa inatendeka kwa kutafsiri ujumbe jinsi ulivyo kutoka LC hadi LL. Hii ilitusaidia kwa kuangalia urasmi wa mahakama wa kutumia msamiati maalum katika kuwasilisha hoja katika mahakama jambo ambalo huleta matatizo.

Kwa upande mwingine chanzo cha matatizo ya ukalimani ni wale wanaokalimaniwa. Hale (2004) anabainisha kuwa wanaokalimaniwa hasa wasioelewa LC pia huwa hawaelewi wajibu wa mkalimani na hivyo hutarajia kuwa mkalimani kazi yake ni kutoa mwongozo, mashauri au usaidizi. Iwapo mkalimani atahisi kuwa kazi yake ni kufanikisha mawasiliano atawajibika kufanya marekebisho katika baadhi ya matamko ili kuboresha uelewaji vyema. Hii ilitusaidia katika kubainisha aina ya matatizo ya tafsiri na ufasiri.

Cremona na Mallia (2004) Wataalamu wa ukalimani katika mikutano ya kimataifa wanasema dhana tafsiri na ukalimani zina uhusiano mkubwa. Wanatoa maelezo yanayoonyesha tofauti kati ya mtafsiri na mkalimani. Wao wanasema kwamba mtafsiri hufanya kazi pekee akiwa na karatasi pamoja na matini. Wao huiunda upya matini hiyo sawa na mtunzi wa pili kwa kuelewa na kuunda upya stadi za mwandishi asilia. Mkalimani kwa upande mwingine hufanya kazi katika hali ya upweke. Yeye hufanya kazi pamoja na mnenaji ambaye wakati mwingine hufafanua mada yake na kueleza fikra moja kwa moja bila kumpa mkalimani wakati wa kutoa ufafanuzi upya au kutafuta visawe mwafaka. Mkalimani huwa na hadhira ambayo humsikiliza sawia na yule mnenaji. Muda huwa mfupi sana kati ya tamko la mnenaji na la mkalimani. Jambo hili lawezesha kuleta uwezekano wa mkalimani asiye makini kutumia maneno yasiyofaa ili kuepuka kusubirisha hadhira yake. Utumizi huu wa maneno yasiofaa ulichunguzwa katika utafiti huu ili kubainisha kama ukalimani una maneno mengi yasiowakilisha dhana kama ilivyo katika lugha chanzi. Utafiti wao unahusiana na ukalimani unaofanywa katika nyanja za kidiplomasia katika muktadha huo wakalimani huwa watu waliohitimu katika kazi hiyo na huteuliwa kwa makini. Katika utafiti huu, waliofanya tafsiri na ufasiri walikuwa ni makarani ambao hawakuwa wamepewa mafunzo kabambe kuhusu tafsiri na ukalimani. Isitoshe, utafiti huu ni muhimu kwa sababu mkalimani alifanya tafsiri na ufasiri jambo ambalo tulishughulikia katika kubainisha chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri.

2.3 Msingi wa nadharia ya tafsiri ya Nida

Kulingana na Nida, (1964) nadharia ya tafsiri ni sheria ama taratibu ambazo mfasiri anahitajika kuzifuata ili kupata ujumbe uliokusudiwa kutoka kwa LC hadi LL. Nida anasema tafsiri ni taaluma ya Sayansi kwa sababu ina utaratibu ambao unahitajika kufuatwa kwa mtu yeyote yule anayetaka kufanya utafiti. Kigezo cha sheria basi ni muhimu sana kupata maana kutoka LC hadi LL katika nadharia hii. Nadharia hii imejengwa katika mihimili ifuatayo.

1. Tafsiri inapaswa kuchukuliwa kama taaluma ya kisayansi.
2. Lugha ni zao la utamaduni na kwamba matatizo yote yanayokumba tafsiri yana msingi wake katika mazingira na tamaduni za lugha hizo mbili.
3. Anayetafsiri awe na sifa mahsusi

Mihimili hii ilitusadia katika utafiti. Mhimili wa Kwanza, tafsiri kama taaluma ya kisayansi ina maana kwamba ukalimani lazima ufuate utaratibu maalumu. Katika utaratibu huo kuna haja ya kutambua tatizo, kujitokeza na malengo, kuorodhesha au kujitokeza na mbinu za kufanyia uchunguzi ili kutatua tatizo hilo, kufanya uchunguzi wenyewe na kujitokeza na ripoti ya uchunguzi huo. Pia kuna tatizo ambalo ni ukosefu wa maelewano kati ya watu ambao wana nia ya kuelewana. Kulingana na nadharia hiyo lazima kuwe na mbinu za kufanya ukalimani ili kuwawezesha hao kuwasiliana. Baada ya ukalimani kufanywa kuna haja kuitathmini ili kuona kama matokeo yake yameafikiana na lengo la kufanya ukalimani huo. Katika ukalimani utaratibu unapaswa kuwa huohuo mmoja. Katika utafiti huu, mkalimani anatarajiwa kuelewa kuna makundi mawili katika hadhira ambayo hayaelewani na kwamba ni kazi yake kufanya waelewane. Baada ya kufanya ukalimani ni vyema kutathmini kazi hii. Mtafiti alitathmini kwa kuwauliza hadhira iwapo washtakiwa walifaidika na ukalimani. Hii ndio maana utafiti huu ulichukulia maoni ya hadhira kuwa ni muhimu katika kujua walivyopokea ujumbe uliofasiriwa. Maoni hayo yalichukuliwa kama tathmini ya ubora wa ukalimani.

Pia, tulizingatia mhimili wa pili kuwa lugha ni zao la utamaduni. Tungependa kuongezea kuwa katika msingi huu mfasiri alihitajika kuzingatia mwelekeo wa lugha yaani anaelemea upande wa lugha chanzi au lugha pokezi. Nida alieleza kuwa lugha lazima ijikite katika utamaduni. Hali hiyo huzua swala la mawasiliano kati ya watu wasiotumia lugha moja na ambao hutoka katika mazingira na tamaduni tofauti, baadhi ya matatizo hayo ni kama vile kutafsiri kijuujuu, kuyahepa baadhi ya maneno, kutopata uwiano halisi kwa sababu ya tofauti za kimazingira, utamaduni wa vifaa, wa jamii, wa kidini, na wa lugha.

Utafiti huu ulichunguza matatizo katika ujumbe katika kalimani. Kama alivyosema Nida matatizo haya huenda yanatokea kwa sababu ya tofauti za kimazingira kati ya lugha za Kiingereza na Kiswahili. Nida anasema tofauti za kimazingira huleta matatizo katika kuyapata maneno yanayofanana au yanayowasilisha dhana moja. Miundo ya lugha tofauti pia huweza kuleta matatizo. Ili kufanikisha mawasiliano mtu anayetafsiri kutoka lugha moja hadi nyingine wakati mwingine hulazimika kutumia kirai katika lugha lengwa kuwasilisha dhana ambayo katika lugha chanzi ni neno moja tu. Kwa mfano katika Kiingereza "Dry cow" ikitafsiriwa moja kwa moja katika Kiswahili "Ng'ombe aliyekauka" huleta maana tofauti kabisa. Wao waingereza wakimaanisha "Ng'ombe aliyeacha kutoa maziwa". Dhana hiyo inaweza kueleweka katika Kiswahili lakini kwa kutumia maneno mengi. Brown (1995) anapendekeza kuwa ni muhimu

suala la ukalimani linapofanywa nia ya msemaji ifikiriwe. Brown anasema kuwa pia msikilizaji au msomaji husikiliza akiwa na nia fulani.

Katika mahakama iwapo mshtaki ametumia neno moja, huenda akafikiria kuwa neno hilo linakalimanika moja kwa moja na kufasiri katika LL. Hali hii inaweza kumfanya kuendelea kuongea bila kuelewa kwamba maneno machache aliyoyatumia yanahitaji maelezo marefu katika lugha lengwa. Jambo hili linaweza kuleta matatizo kwani mkalimani hatakuwa na muda wa kutosha wa kueleza yanayosemwa na mshtaki au mshtakiwa.

Misingi hii iliyoorodheshwa na Nida ilitusaidia katika kuweka vigezo vya kutumia wakati wa kuchanganua deta yetu ili kuainisha matatizo yanayojitokeza pamoja na umaratokezi wake katika deta hiyo. Utamaduni wa lugha kama unavyoelezwa na Nida ulitusaidia kuchanganua matamko yaliyokalimaniwa katika viwango vya Leksia na Sintaksia. Matatizo ya kimaana yanahitaji kuangaliwa kwa uangalifu mkubwa katika mktadha wa matumizi. Katika utafiti wetu tulikumbana na tamaduni mbili: tamaduni za Kiswahili na Kiingereza. Hii ina maana kwamba mfasiri atafanikiwa kuwasilisha ujumbe katika tafsiri yake anapofahamu tofauti na mawiano ya kitamaduni yanayowakilishwa na lugha zinazohusika. Hii ilituongoza kwa kulinganisha utamaduni mbili wa Kiingereza na Kiswahili na kuangalia jinsi mkalimani alivyofasiri matamko katika mazingira ya mahakama. Kwa kuchunguza matamko, neno au maana ilivyofasiriwa dosari zilizojitokeza ndiyo mambo tuliyochunguza.

Mhimili wa tatu pia, ulituongoza katika utafiti huu kwa kuangalia chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama. Katika msingi huu Nida alizungumzia sifa ambazo zinamfaa mfasiri. Sifa hizo hizo ni:

1. Mfasiri awe na ufasaha wa lugha zote mbili zinazohusika katika tafsiri. Ilimsaidia mtafiti kutambua makosa kwa sababu ya ujuzi wa lugha.
2. Azijue tamaduni zote mbili za lugha zinazohusika
3. Mfasiri lazima ajue isimu nadharia za lugha zote mbili zinazohusika katika viwango vya sauti, mofolojia, msamiati, sarufi na maana. Hii ilimsaidia mtafiti kusoma ili kutambua iwapo kuna tofauti katika mtindo au umbo katika lugha hizi mbili.
4. Mfasiri lazima ajue aina za tafsiri: Tafsiri ya neno kwa neno, tafsiri ya sisisi, tafsiri maana na tafsiri mawasiliano. Hii ilimsaidia mtafiti kujua faida au udhaifu wa kila aina ya tafsiri mkalimani atumiayo. Hii ina maana kuwa namna yoyote ya tafsiri isiwe yenye kuelemea upande mmoja tu.

5. Mfasiri lazima ajue aina za tafsiri.
    I. Sikiliza matamko kwa makini ili kuhakikisha umeelewa vyema yote yaliyomo na maudhui yake.
    II. Unatafuta maana sawa au iliyokusudiwa katika LC hadi LL.
    III. Unaubadiliisha ujumbe uliokusudiwa kutoka LC hadi LL huku ukifadhi utamu na usahihi wa lugha.

Sifa hizi zilikuwa muhimu katika utafiti huu kwa sababu tulichunguza wakalimani ili kujaribu kubainisha kama kulikuwa na uhusiano kati ya ujuzi wao na mafunzo waliyopata. Baadhi ya mambo ambayo Nida ametaja kama isimu nadharia na aina za tafsiri yanaweza kupatikana miongoni mwa watu waliopata mafunzo kuhusu kazi hiyo.

Nadharia ya tafsiri ni muhimu kwa mfasiri kwa kuwa inasaidia kwa kudokeza ni mambo gani yazingatiwe katika tafsiri. Katika utafiti huu, tulitarajia mkalimani kuuzingatia ujumbe ulivyowasilishwa kwake bila kubadilisha ujumbe. Mfasiri alihitaji kuwafahamu anaowafasiria pamoja na mazingira yake. Huhitajika pia, kufahamu kiwango cha elimu, tabaka au umri ili ajue vipi atakavyofasiri. Haya ambayo tumetaja ni utaratibu wa kufuatwa katika tafsiri. Tulitumia mhimili huu kwa kuchunguza ni kwa njia ipi mfasiri alitekeleza majukumu yake katika kazi yake. Iwapo hakuzingatia ujumbe uliopo katika matamko basi tafsiri aliyotoa ilipotosha. Hivyo basi, hayo ndiyo matatizo tuliobainisha katika kazi yetu.

SURA YA TATU
MBINU ZA UTAFITI

3.1 Utangulizi

Mtafiti amegawa sura hii katika sehemu mbalimbali: sehemu hii inahusu muundo wa utafiti, eneo la utafiti ambapo utafiti ilifanywa, uteuzi wa sampuli. Katika sura hii, mtafiti ameeleza kwa kirefu mbinu na hatua alizozingatia katika ukusanyaji wa deta yake kwa kuangazia mahojiano, matamko na viziada Lugha. Isitoshe uchanganuzi wa deta iliyokusanywa ulifanywa.

3.2 Muundo wa utafiti

Utafiti huu umechukua muundo wa kimaelezo. Kwa mujibu wa Hughes (1989) na Merriam (1998), utafiti wa kimaelezo huwa bora katika kuelezea mitazamo ya watu kuhusu jambo, au maana wanalipa suala hilo. Bryman (2001) amejadili umuhimu wa utafiti wa kimaelezo katika kutoa habari nyingi na za kina kwa wahojiwa. Aidha, utafiti wa kimaelezo hutoa maelezo halisi ya jinsi jambo lilivyo na hutumika katika kufafanua tabia na mitazamo ya wahojiwa (Mugenda, 2003). Ufafanuzi huu kuhusu utafiti wa kimaelezo unaafikiana na suala la utafiti huu.

3.3 Eneo la utafiti

Utafiti huu ulifanywa katika mahakama ya Kitale ambao ndio mji mkuu wa kaunti ya Trans-Nzoia. Mahakama ya Kitale ni mojawapo ya mahakama katika eneo la kaskazini mwa mkoa wa Bonde la Ufa hivyo basi, huhudumia wananchi wa sehemu kutoka Lodwar, Pokot magharibi, Trans-Nzoia, Uasin-Gishu na Sehemu za wilaya ya Bungoma. Ingawa kuna mahakama ya chini ya Lodwar na Kapenguria kesi ambazo hazisikizwi hapa hufanyiwa mahakama ya sheria ya Kitale. Mahakama ya sheria ya Kitale ni mojawapo ya mahakama makuu nchini ambapo kuna mahakama kuu na vilevile ya chini. Iwapo mshitakiwa baada ya hukumu kutolewa hajaridhika na uamuzi wa hakimu anaweza akakata rufaa katika mahakama ya Eldoret, Nakuru au Nairobi. Deta iliyokusanywa iliwakilisha baadhi ya mambo yanayotokea katika mahakama mengine nchini hasa katika kesi ambapo ukalimani hufanywa. Aidha, ilipunguza gharama kwa sababu utafiti haungeweza kufanywa katika mahakama yote nchini.

3.4 Uteuzi wa sampuli

Uteuzi wa Sampuli ulikuwa wa kimaksudi na pia mbinu ya uchunguzi ilitumika katika kupata matamko ambayo yalifasiriwa kutoka kesi za jinai ambapo ukalimani unafanywa. Matamko hayo ni kutoka kwa mshtaki na mshtakiwa. Mahakama ya Kitale ina jaji mmoja, mahakimu watano na mawakili 32 na karani 24. Mahakama hii ina aina 5 za vikao tofauti ambapo kesi husikilizwa. Mtafiti alijikita kimaksudi katika korti tatu ya 1, 3 na 5. Idadi hii ni mwafaka kwa sababu inawakilisha asilimia 60 ya idadi. Pia idadi ya wakalimani 9 iliwakilisha asilimia 37.5 ya idadi (24). Idadi hizi zilizoteuliwa ni mwafaka kwa kutoa habari za kina (Mugenda, 2003). Mtafiti alikusanya matamko katika shughuli za mahakama ambapo ukalimani ulifanyika mara tatu katika kila korti ili kukusanya deta; hivyo kunasa vikao tisa vilivyokalimaniwa. Idadi hii ni mwafaka kwa kuwa uchanganuzi wa kina ungefanyika. Lovejoy (1991) na Bazerman (1981) wanasema kuwa makala 3 yanatosha lakini kwa minajili ya utafiti huu, idadi ni juu ili kuzingatia viwango mbalimbali vya mahakama hii ya Kitale.

3.5 Ukusanyaji deta

Nyenzo zilizotumika katika kukusanyia deta ilikuwa ni mahojiano na kurekodi matamko kwa kinasa sauti. Vilevile mbinu ya uchunguzi wa kawaida ulitumika katika kuchunguza viziada lugha vilivyojitokeza katika shughuli za mahakama. Katika viziada lugha letu ilikuwa maswala ya lugha.

3. 5.1 Mahojiano

Watafiti wengi kama vile: Kothari (2003), Ogula (2003) na Seal (2004) wameelezea umuhimu wa mahojiano kama mbinu ya utafiti inayoweza kutumiwa katika kujua mitazamo ya watu na yale wanayothamini. Wataalamu hawa wamefafanua kuwa haya ni mambo yasiyoweza kujulikana kwa kutumia hojaji ya kawaida. Mutai (2000) na Bryman (2001) wanaona mahojiano kama mbinu bora zaidi ya kupata majibu ya kina kutoka kwa wahojiwa.

Kwa manufaa ya utafiti huu, dodoso iliandaliwa kwa wakalimani walioteuliwa katika mahakama ambapo ukalimani ulifanywa. Dodoso hii ililenga kufahamu mtazamo wa wakalimani kuhusu ukalimani, kubainisha ufahamu wa wakalimani kuhusu majukumu, elimu yao, tajriba na mengineo. Rejelea kiambatanisho A uk. 65.

Isitoshe, hadhira ilihojiwa. Katika kila kikao ambacho mtafiti alinasa matamko mtu mmoja kutoka hadhira alihojiwa kutathmini jinsi mkalimani alivyotekeleza ukalimani.

Katika utazamaji wa kawaida tulichunguza mshtakiwa na mshtaki jinsi walivyotumia viziada lugha. Tulichunguza:

1. Ishara za kutumia mikono
2. Kutikiza kichwa
3. Vilio
4. Vicheko
5. Vidatu

Wahusika katika mktadha mbalimbali hutumia viziada lugha na sifa za kiarudhi zinazotofautiana. Sifa hizi ni: Toni za sauti zao, kidatu, kuashiria mazungumzo na kusita. Haya hutumiwa kuimarisha ushikamano na ushirikano katika maongezi. Sifa hizi zilitumiwa kuonyesha nini kinachotangulia na nini cha kurejelewa; nini kisababishi na matokeo ya mazungumzo fulani. Halafu kuthibitisha misimamo ya yote yanayowasilishwa kutoka kwa mzungumzaji hadi kwa msikilizaji. Tulichunguza viziada lugha ambavyo vilionyesha uhusiano kati ya wahusika katika mazungumzo. Tulichukulia kuwa aidha utamaduni wa watu wa maeneo sawa huonyesha kuwa vingi vya viziada lugha hujulikana miongoni mwao. Kwa ujumla viziada lugha hivi vilitumika kuonyesha kuhesabu, kuitikia na kukataa. Katika utafiti huu ilibidi kujua viziada hivyo vilimaanisha nini. Isitoshe, ilibidi kuandika nini walichokusudia katika ishara walizotumia. Uchunguzi huu ulikuwa muhimu kwa kuwa (Bolinger, 1980) amedokeza kuwa wanajamii wanapotazamana, kutumia miondoko ya kichwa, ishara za mkono na viganja, sura zao, hatua kati yao wanapozungumza, wanapokohoa, kelele na kimya kati yao haya yote ni njia ya mawasiliano katika mila au utamaduni huo.

3.5.2 Uchanganuzi wa matamko yaliyorekodiwa

Matamko ya shughuli za mahakama yalinaswa katika kinasa sauti. Mtafiti alihudhuria shughuli za mahakama ya Kitale ili aweze kunasa matamko 9 yaliyokalimaniwa. Isitoshe, katika vikao ambapo ukalimani ulifanywa hadhira ilihojiwa. Wasailiwa wanaoelewa Kiingereza na Kiswahili waliteuliwa kimakusudi. Katika kila kikao msailiwa mmoja aliteuliwa hivyo kuwa na wasailiwa 9. Mbinu hii ya mahojiano ni bora kwa sababu mtafiti huingiliana na wahojiwa hivyo

kupata deta kwa kina (Mutai, 2000). Maswali yalikuwa wazi na funge yaliyomwongoza msailiwa katika kujibu yanayohusu mada ya utafiti.

Matamko yalipewa nambari C1 hadi C9 ili yawe rahisi yanaporejelewa. Kwa mujibu wa Mills (1999), wachanganuzi usemi hamu yao kubwa ni kuchunguza lugha kama inavyojitokeza katika matamko yaliyonaswa kwa kinasa sauti au matini yalivyoandikwa. Ogula (2003) amependekeza ufaafu wa mbinu hii katika kutoa habari sahihi kutokana na kutoathiriwa na kile kinachochanganuliwa. Kwa kufanya hivyo mtafiti aliweza kutazama jinsi maneno yalivyotumika na maana iliokusudiwa, aina ya makosa yaliyotambuliwa, idadi yake na jinsi yalivyofasiriwa.

Mtafiti alitumia wafasiri wachache aliofanya urafiki nao ili kuwapata makarani wengine kwa kuwateua kimakusudi kutoka wa kwanza hadi nambari tisa (Milroy, 1987). Uteuzi wa wasailiwa ulikuwa wa kimakusudi. Mbinu hii ni muhimu kwa sababu huwezesha kufanya uchunguzi wa kina wa jambo linalotafitiwa (Kombo na Tromp 2006). Mtafiti alifanya utafiti wa majaribio na akatambua kuwa maswali yalikuwa mwafaka katika utafiti. Isitoshe mtafiti alitambua kuwa wasailiwa hawakutaka majina yao yatajwe na siri zote zilihitajika kuhifadhiwa. Mtafiti kazi yake ilikuwa ni kutambua matatizo ya ukalimani na kuyaacha masuala mengine nyeti kwa watalaamu wa sheria jambo alilozingatia katika utafiti wake. (Silverman, 2005).

3.6 Uchanganuzi wa deta

Uchanganuzi wa deta ulifanyika kwa mujibu wa nyenzo za utafiti zilizokuwa zimeandaliwa awali. Deta ilikuwa matamko yaliyofasiriwa pamoja na majibu ya wasailiwa.Tunukuzi tisa ambazo zilikamilika ndizo zilizoshughulikiwa. Hizi ndizo zilisikika vyema. Ziliandikwa kwa lugha ya Kiingereza na Kiswahili kwa mwambatano. Zilichanganuliwa kwa kuzingatia mihimili ya nadharia ya Nida. Nadharia ya Nida ilimsaidia mtafiti kuelewa jinsi matatizo yanavyohusishwa na utamaduni wa lugha mbili zozote zile na hivyo kuangalia tofauti za kimazingira na utamaduni katika mahakama. Swala la mfasiri awe na ufasaha wa lugha mbili ulimsaidia kulinganisha matamko ya lugha hizi mbili ili kutambua makosa. Kujua aina mbalimbali ya ukalimani kulimwezesha mkalimani kujua faida na upungufu wa kila aina ya tafsiri. Kujua isimu nadharia za lugha zote mbili kulisaidia kutambua tofauti katika mtindo au umbo katika lugha hizi mbili hivyo basi kuzua matatizo. Kujua hatua za ukalimani kulimsaidia mkalimani kusikiza matamko kwa makini na kutamka ipasavyo na kuhamisha ujumbe ipasavyo kutoka LC hadi LL. Iwapo hangezingatia haya basi kungekuwa na matatizo. Matatizo haya ni ya

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

udondoshaji ambapo matamko yaliachwa, matatizo ya nyongeza ambapo neno au maneno yaliongezwa ambapo hayakukusudiwa kuwa katika LC. Matatizo ya utamaduni ni yale yaliyotokea kwa sababu ya tofauti za kiutamaduni na mazingira ya lugha hizi mbili hivyo kukosa visawe mwafaka. Matatizo ya ujumbe uliopotoka yalitokea kwa sababu ya tofauti katika maumbo ya lugha hizi mbili au matatizo ya kileksia kwa kutumia neno lisilofaa hivyo kupotosha ujumbe au mkalimani kuliacha bila kulitafsiri.

Majibu kutoka kwenye mahojiano ya wasailiwa na hadhira yalirekodiwa kisha yalichanganuliwa na maelezo yakatolewa kupitia kwa takwimu na majedwali. Uchanganuzi ulitolewa kwa njia ya maelezo ya moja kwa moja kutokana na majibu ya wahojiwa. Aidha, takwimu zilitumika kuelezea asilimia au idadi ya kutukia kwa majibu ya wahojiwa. Hatimaye matokeo ya utafiti yalitolewa kupitia kwa maelezo, majedwali na takwimu.

SURA YA NNE

UWASILISHAJI, UCHANGANUZI NA UFASIRI WA DETA

4.1 Utangulizi

Sura hii inaelezea uchanganuzi wa deta zilizotokana na mahojiano ya wasailiwa, na uchanganuzi wa matamko ya ukalimani yaliyonaswa mahakamani. Mtafiti alitumia mbinu ya mahojiano katika kupata deta. Pia mbinu ya uchunguzi katika kunasa matamko yaliyokalimaniwa. Deta ilichanganuliwa kwa kina kwa kutazama msamiati na maana ilivyojitokeza katika sentensi, usemi au matamko.

Uchanganuzi wa deta umegawanywa kwenye sehemu tatu. Sehemu ya kwanza inalenga maoni ya ukalimani kutokana na mahojiano. Sehemu ya pili ni matokeo ya miitikio ya hadhira waliohudhuria shughuli za mahakama ambapo ukalimani ulifanywa. Sehemu ya tatu inashughulikia uchanganuzi wa matamko yaliyokalimaniwa.

4.2 Maoni ya wakalimani kuhusu ukalimani kutokana na Mahojiano

Mwongozo wa maswali ulihusu taarifa za kimsingi na maoni mbalimbali kuhusu ukalimani na tafsiri. Rejelea kiambatisho A uk. 65.

4.2.1 Taarifa za kimsingi

Katika kitengo hiki, wasailiwa walihitajika kutoa maelezo kuhusu jinsia yao, umri wao, elimu na tajriba katika ukalimani. Deta ilikusanywa kutoka kwa wasailiwa 9.

4.2.2 Jinsia ya wakalimani

Ilibainika kuwa kati ya wasailiwa 9 waliohojiwa 4 walikuwa ni wanawake hii ikiwa ni 44.44% ya wasailiwa na 5 wanaume hii ikiwa ni 55.56%. Matokeo yaliwekwa katika jedwali 1

Jedwali 1: Jinsia ya wakalimani

Jinsia	Idadi	Asilimia %
Wake	4	44.44
Waume	5	55.56
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

4.2.3 Umri wa wakalimani

Katika kitengo hiki wasailiwa walitoa umri wao. Matokeo yameonyeshwa katika jedwali 2.

Jedwali 2: Umri wa wakalimani

Umri	Idadi	Asilimia %
Chini ya miaka 20	0	0
Miaka 20-25	1	11.11
Miaka 26-30	2	22.22
Miaka 31-35	2	22.22
Miaka 36-40	3	33.33
Zaidi ya maka 41	1	11.11
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Ilibainika kuwa hatukuwa na mkalimani aliyekuwa chini ya umri wa miaka 20. Asilimia 11.11 walikuwa na miaka 20-25, asilimia 22.22 miaka 26-30, asilimia 22.22 miaka 31-35, asilimia 33.33 miaka 36-40 na asilimia 11.11 zaidi ya miaka 41. Matokeo haya yalionyesha kuwa wakalimani waliokuwa na umri wa miaka 36-40 ndio waliokuwa wengi kisha kadiri miaka ilipoongezeka wakalimani walipungua.

4.2.4 Elimu ya wakalimani

Wakalimani waliohojiwa walibainisha viwango vyao vya masomo vya kiwango cha juu walivyohitimu. Matokeo yameonyeshwa katika jedwali 3

Jedwali 3: Elimu ya wakalimani

Elimu	Idadi	Asilimia %
Uzamili	0	0
Chuo kikuu	0	0
Kidato cha sita	2	22.22
Cheti cha Shahada	7	77.78
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Jedwali hili linaonyesha kuwa wasailiwa wengi waliohojiwa waliokuwa na cheti cha shahada ya kidato cha nne. Wao waliwakilisha 77.78 % ya wakalimani. Asilimia 22.22 walikuwa na vyeti vya kidato cha sita. Utafiti ulionyesha kuwa hatukuwa na wafasiri waliokuwa na elimu ya chuo kikuu au uzamili. Isitoshe, waliajiriwa kama makarani lakini kukiwa na haja ya kufasiri walifanya kazi hii. Walihatajika kujua lugha ya Kiingereza, Kiswahili na lugha ya Mama yoyote ile ili kukitokea haja ya mhusika ambaye hafahamu lugha inayotumika wakati huo basi atafanya ufasiri. Ilibainika kuwa kabla ya kuanza kazi hii ya ukalimani ulihitajika kula kiapo cha uaminifu mbele ya jaji.

4.2.5 Tajriba katika ukalimani

Tulichunguza tajriba ambayo kila mkalimani alikuwa nayo. Wasailiwa 9 waliohojiwa walikuwa na tajriba mbalimbali. Tajriba ilionyesha kipindi cha miaka ambapo mkalimani alifanya kazi (miaka ambayo amefanya kazi ya ukalimani). Tazama jedwali 4

Jedwali 4: Tajriba katika ukalimani

Tajriba katika ukalimani	Idadi	Asilimia %
Chini ya mwaka mmoja	0	0
Mwaka 1-3	1	11.11
Mwaka 4-6	2	22.22
Mwaka 7-10	5	55.56
Zaidi ya miaka 10	1	11.11
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Jedwali hili linaashiria kuwa hatukuwa na mkalimani aliyekuwa amefanya ukalimani chini ya mwaka mmoja. Katika kitengo cha mwaka 1-3 kulikuwa na 11.11%, mwaka 4-6, 22.22%, mwaka 7-10 asilimia 55.56 na walio na zaidi ya miaka 10 asilimia 11.11. Wafasiri waliokuwa na tajriba ya mwaka 7-10 walikuwa ndio wengi kwa asilimia 55.56. Mtafiti hakuchunguza kwa undani iwapo tajriba huchangia katika kuwa na ufasiri bora lakini katika matokeo ya mtafiti labda kulikuwa na uwezakano kwani walichukuliwa kuwa wao ndio wana ujuzi kabambe kwa sababu ya kufanya kazi hii kwa muda mrefu. Walikuwa na umahiri kwa sababu ya kufanya kazi

katika mazingira ambayo sajili haibadiliki. Sajili hii ya sheria basi inaeleweka kwao kwa sababu maneno ni yale yale na iwapo wameyasikia na kutafsiri kwa muda mrefu huenda tafsiri zikawa bora zaidi. Mtafiti alitarajia kuwa basi waliokuwa na tajriba ya zaidi ya miaka 10 wangekuwa wengi lakini ilibainika kuwa waliokuwa na tajriba hii walipandishwa vyeo na kutekeleza majukumu mengine kortini na hivyo hawakufasiri tena katika mahakama.

4.2.6 Kozi za ukalimani

Matokeo ya mahojiano ya wakalimani yalitusaidie kutambua aina za kozi walizokuwa wamefanya kabla ya kuajiriwa zinazohusiana na ukalimani. Tazama jedwali 5

Jedwali 5: Kozi za ukalimani

Kiwango cha kozi	Idadi	Asilimia %
Chuo kikuu	0	0
Diploma	0	0
Cheti cha shahada	0	0
Warsha/semina/kongamano	2	22.22
Nyingine	7	77.78
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Kwa wasailiwa wote waliohojiwa asilimia 22.22 ilionyesha kuwa walihudhuria aidha semina, kongamano au warsha hata hivyo wote walikiri kuwa mikutano hiyo haikushughulikia masuala ya ukalimani kwa kina. Kozi hizi zilihusu masuala kama vile kuinua viwango vya uwajibikaji kazini na masuala ya uhusiano mwema katika kazi. Matokeo pia, yalionyesha kuwa hatukuwa na wakalimani ambao walikuwa wamehudhuria kozi za shahada katika chuo kikuu au Diploma au cheti katika ukalimani. Asilimia 77.78 ya wakalimani walitumia mbinu nyingine kama vile kusoma majarida, kusoma makala ya wenzao ambao walikuwa wamefanya mtihani wa kuboresha kazi yao. Isitoshe, mitihani haikuwa na silabasi mahsusi. Pia, kozi hizi zilinuia kuboresha viwango vya uongozi, masuala ya uhasibu na mengineo. Iwapo yeyote angelipita mitihani hii kulikuwa na uwezekano wa kumpandisha kutoka cheo kimoja hadi kingine baada ya miaka 3.

4.2.7 Maoni ya wakalimani kuhusu mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani

Wasailiwa walitoa maoni mbalimbali kuhusu haja ya mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani. Tazama jedwali 6

Jedwali 6: Maoni kuhusu mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani

Kauli	Idadi	Asilimia %
Kuna haja ya mafunzo	7	77.78
Hamna haja ya mafunzo	2	22.22
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Asilimia 77.78 ya wakalimani walisema kuwa kulikuwa na haja ya makarani kupewa mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani kwa sababu zingeliwasaidia katika kuboresha ukalimani na kuelewa zaidi sajili ya sheria katika kutambua aina za ukalimani, matatizo mbalimbali katika ukalimani baadhi ya mambo mengine. Mbinu mwafaka za ukalimani zingeliwasaidia kuelewa mambo ya kuzingatia katika kazi yao. Hili lingeliboresha viwango vya kujua lugha katika kujieleza. Kwa upande mwingine, asilimia 22.22 waliona haikuwa na haja ya kufunzwa mafunzo ya sheria au mbinu mwafaka kwa sababu kazi ya ukalimani haikuchukuliwa kuwa ngumu. Wao waliamini iwapo unaelewa lugha mbili husika hilo linatosha waliamini pia kuwa kazi hii iliendelea kuwa nyepesi kadri unavyokuwa na tajriba na hasa unapoelewa masuala ya sheria pamoja na urasmi unaofuatwa mahakamani.

4.2.8 Maoni kuhusu ufahamu wa wajibu / majukumu ya mkalimani

Katika sehemu hii wasailiwa walitoa maoni mbalimbali kuhusu wanavyotekeleza kazi ya ukalimani. Maoni yao yalihusu ufahamu wa majukumu yao.Tazama jedwali 7

Jedwali 7: Maoni kuhusu ufahamu wa majukumu / wajibu wa mkalimani

Jukumu /wajibu	Idadi	Asilimia %
Kufanikisha mawasilano	5	55.26
Kuratibu na kufasiri	1	11.11
Kufasiri neno kwa neno	1	11.11
Kuwasaidia washtakiwa kuelewa matamko vizuri	2	22.22
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Ilibainika kuwa asilimia 55.56 ya wakalimani waliohojiwa walitoa maoni kuwa wao hufanya ukalimani ili kufanikisha mawasiliano, 22.22% waliamini kuwa jukumu la mkalimani ni kuwasaidia mshtakiwa ili kushinda kesi, asilimia 11.11 walikubaliana kuwa jukumu la mkalimani ni kuratibu na kufasiri, 11.11% ilitoa maoni kuwa jukumu la mkalimani ni kufasiri neno kwa neno.

4.2.9 Maoni kuhusu matayarisho wanayofanya kabla ya ukalimani

Wakalimani walitoa habari kuhusu maandalizi wanayofanya kabla ya ukalimani. Haya yameonyeshwa katika jedwali 8.

Jedwali 8: Maoni kuhusu matayarisho wanayofanya kabla ya ukalimani.

Matayarisho	Idadi	Asilimia %
Kusoma istilahi za kortini	2	22.22
Kutambua taratibu za kortini	1	11.11
Kuwa na uelewa wa lugha husika	1	11.11
Hamna matayarisho	5	55.56
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Wasailiwa walipohojiwa iwapo wao hujitayarisha kabla kufanya ukalimani, asilimia 55.55 walikiri kuwa huwafanyi matayarisho yoyote mradi ufike tu mahali ambapo kesi inafanywa kwa

wakati ufao. Isitoshe huwa hamna maandalizi ya awali kuwa siku hiyo. Asilimia 22.22 walikiri kuwa wao husoma na kufahamu istilahi za kortini. 11.11% walikiri kuwa matayarisho ambao wao hufanya ni kutambua utaratibu wa kortini kwa kumwelekeza mshtakiwa kile anachohitajika au kumwongoza kujibu maswali ipasavyo. Asilimia 11.11 ilikiri kuwa kulikuwa na haja ya kuelewa lugha husika kwa kuangalia kwa kina kile kilichokuwa kinajadiliwa.

4.2.10 Maoni ya washtakiwa / washtaki kuhusu ukalimani

Wasailiwa walipohojiwa ikiwa washtaki / washtakiwa iwapo hulalamika kuwa kile kilichotafsiriwa sicho walichokusudia kusema asilimia 100 walikiri kuwa hilo kuwa halitokei hata hivyo wasailiwa walikiri kuwa wengi iwapo hawajaelewa sehemu fulani huuliza mkalimani arudia tena au wengine hunyamaza kimya lakini mwishowe husema kuwa walionewa na mahakama.

4.2.11 Maoni kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wakalimani

Wakalimani pia walihitajika kutoa habari kuhusu changamoto wanazokumbana nazo katika kazi hii ya ukalimani. Tazama jedwali 9

Jedwali 9: Maoni kuhusu changamoto wanazokumbana nazo wakalimani

Changamoto	Idadi	Asilimia %
Ukosefu wa visawe	2	22.22
Istilahi za sajili ya sheria	1	11.11
Ukosefu wa mafunzo kabambe	1	11.11
Malipo duni	5	55.56
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Kutokana na jedwali 9, asilimia 55.56 ya wakalimani walikiri kuwa changamoto kubwa ni malipo duni, asilimia 22.22, ukosefu wa visawe wanapofasiri, asilimia 11.11 istilahi za sajili ya sheria na asilimia 11.11 ukosefu wa mafunzo kabambe.

4.2.12 Maoni jinsi ya kukabiliana na matatizo

Wakalimani walihitajika kutoa maoni yao jinsi ya kukabiliana na matatizo mbalimbali. Katika matatizo ya ukosefu wa visawe mwafaka walipendekeza kuwa wao hutumia maneno yaliyokaribu na maana iliyokusudiwa. Aidha walikiri kuwa wakati mwingine wao hukwepa maneno haya magumu. Katika tofauti za utamaduni na mazingira na maumbo ya lugha mbili wote walikiri kuwa walitumia neno jinsi lilivyo katika lugha chanzi. Pia, walitafsiri neno kwa neno. Katika sehemu ambazo hazikueleweka vyema wakalimani walizipuuza au wakakisia kile ambacho walifikiria mshtaki au mshtakiwa alikusudia kusema.

4.3 Maoni kuhusu tafsiri ya istilahi mbalimbali

Wakalimani walipewa istilahi ili kubainisha jinsi wanavyofasiri. Katika kutambua matatizo mtafiti aliwahoji wafasiri ili watoe baadhi ya maana ya istilahi zinazotumika katika mahakama na jinsi wanavyotafsiri maneno hayo. Majibu yao yaliwekwa katika jedwali 10

Jedwali 10: Tafsiri ya istilahi mbalimbali

Istilahi	**Tafsiri ya istilahi**
Mitigation	Malilio, eleza shida zako, toa shida, eleza korti jambo, jambo la kusema
Defense	Kujitetea, jambo la kusema
Carnal knowledge	Kufanya mapenzi, ngono, kuwa na ufahamu wa sehemu za siri, kubaka
Plea	Mashtaka , maelezo ya mshtakiwa, ombi
Burgulary and Housebreaking	Kuvunja nyumba na kuiba mali ya thamani
Jurisdiction	Uwezo wa korti, mamlaka, eneo
Cross-examinations	Kuuliza maswali
Robbery with violence	Wizi wa mabavu
Confessions	Kukiri, kukubali makosa, tubu, ungama
Indecent assault	Kupapasa, uvamizi, shambulio la nguvu, mapigo, najisi

Asili: Matokeo ya utafiti

4.3.1. Mitigation

Baada ya upande wa mlalamishi au mshtakiwa kutoa ushahidi wao jaji husoma hatia kwa mshtakiwa. Iwapo mshtakiwa hana hatia huachiliwa huru. Akipatikana na hatia jaji husema *mitigation before sentence* Neno hili hutafsirwa kama *Malilio* au *eleza shida zako*. Neno hili hueleweka vyema katika Kiingereza na kwa wanasheria wenyewe. Katika Kiswahili iwapo litachukuliwa na maana tuijuayo hutatanisha mshukiwa kwani mshukiwa huanza kutoa sababu zinazoonyesha jinsi ambavyo hajafanya kosa aliloshtakiwa kwalo badala ya kutoa utetezi ambapo jaji anaweza kumhurumia ili alegeze adhabu atakayoitoa au sababu ambazo jaji anaweza kuzingatia kabla ya kutoa hukumu. Washtakiwa wengi hutoa sababu kama siye mimi nilifanya hivyo au wengine huanza kutoa maelezo kuhusu yaliyotokea. Katika hali hii mshtakiwa anahitajika atoe hoja kama vile ana mke au mume au watoto wanaomtegemea au aeleze jinsi ambavyo iwapo atahukumiwa kifungo jinsi atakavyopoteza kazi au aeleze korti hilo ni kosa lake la kwanza kufikishwa mahakamani. Baadhi ya washtakiwa huanza moja kwa moja kuelezea matukio jambo ambalo huwakera jaji. Ingawa mshtakiwa huelekezwa aeleze shida zake za kibinafsi. Neno *shida* lina maana pana. Kwa mshtakiwa anaweza kuwa na shida za ukosefu wa pesa, ukosefu wa mahitaji ya kimsingi kama vile mavazi, lishe bora au makazi. Iwapo mshtakiwa atajikita na haya itakuwa kazi bure hata kama atahesabu shida ngapi.

4.3.2 Defense

Baada ya ushahidi wote kutolewa kwa upande wa mlalamishi korti huangalia iwapo kuna ushahidi wa kutosha. Korti ikirithika kwamba hakuna ushahidi wa kutosha mshtakiwa huachiliwa huru. Iwapo Korti itaona kwamba kuna ushahidi wa kutosha mshtakiwa hupewa nafasi ya kujitetea. Kwa wakati huu jaji husema "*accused is put on defense*" kuonyesha ana kesi ya kujibu kabla korti haijatoa uamuzi. Wakalimani hutafsiri neno *defense* "*kujitetea*". Katika Kiswahili neno hili hutatanisha kiasi kwamba inabidi mshukiwa afafanuliwe zaidi. Kimsingi mshtakiwa huelezwa kuwa kuna njia tatu za kujitetea. Njia ya kwanza ni kuapa, kulingana na imani ya mshtakiwa, ambapo mshtakiwa huapishwa na baada ya kutoa ushahidi huulizwa maswali na korti au kiongozi wa mashtaka na akiwa na mashahidi aweza kuwaita. Njia ya pili ni pale ambapo mshtakiwa anakosa kuapa, kisha baada ya kutoa ushahidi hataulizwa maswali na korti wala kiongozi wa mashtaka na akiwa na mashahidi pia anaweza kuwaita. Njia ya tatu na ya mwisho, ni pale ambapo mshtakiwa anaweza kunyamaza kimya kungoja korti itoe uamuzi.

Ingawa njia hizi tatu zipo mshtakiwa mara nyingi hajui njia ipi ni bora. Kila mojawapo wa njia hizi zina faida au upungufu wake jambo ambalo wanasheria ndio wanaojua. Kwa mfano njia ya kwanza itatumika tu iwapo mshitakiwa anao ushahidi ambao una uhakika. Washtakiwa wengi hawaelewi wachukue njia ipi na wengi huamua aidha kuchagua hata njia ya pili ili wasiulizwe maswali lakini ushahidi wanaoutoa unakuwa ni dhaifu sana, jambo ambalo lingekuwa bora iwapo wangechukua njia ya kwanza ya kuulizwa maswali ambapo mambo mengine yangewekwa wazi iwapo swali lingeulizwa.

4.3.3 Carnal knowledge

Neno hili lilikuwa na maana nyingi wakalimani wote waliohojiwa walitoa maelezo tu kuhusu neno hili. Wapo waliolitafsiri neno hili kama kufanya mapenzi, wengine walisema kulazimishwa kufanya mapenzi, ngono, kuwa na ufahamu wa sehemu za siri, wengine walitoa maana ya kubaka. Tafsiri hizi zinaonyesha kuwa neno hili lilitumika kwa maana mbalimbali na kwa muktadha mbalimbali. Kwa mfano, katika muktadha ambapo neno litatumika katika hali ambapo mshukiwa anaulizwa kama ana ufahamu wa sehemu za siri anaweza akakubali kosa kwa kujibu ndio huku akichukulia anaelewa sehemu za siri kwa sababu ya kupitia somo la Biolojia au taaluma yake ni udaktari au ameelewa kupitia mtandao. Vilevile, kulazimisha kufanya mapenzi sio sawa na kunajisi. Dhana hizi itabidi zifafanuliwa zaidi. Jambo ambalo lilijitokeza katika kiambatisho C 4.8 uk. 73.

4.3.4 Plea

Neno hili lilitafsiriwa kama kusomewa mashtaka, maelezo ya mshtakiwa kortini, au ombi. Wakati mshtakiwa anafikishwa katika mahakama husomewa makosa yote ambayo ameshtakiwa kwayo. Anahitaji akubali au akatae. Mara nyingine kwa sababu ya kukosa kuelewa washtakiwa hujikuta wamekubali mashtaka ilhali wangelikataa iwapo sehemu ya mashtaka sio sawa.

4. 3.5 Burglary and housebreaking

Maneno haya mawili yalipewa maana kama kuvunja nyumba na kuiba mali ya thamani. *Burglary* lilitumiwa kwa wizi unaofanyika usiku ilhali *housebreaking* ni wizi wa mchana. Dhana ya pili *housebreaking* inaonyesha kwamba mshtakiwa alivunja nyumba kwa nia ya wizi. Anaweza kutekeleza maovu haya wakati wowote hata mchana. Hata pale ambapo hakuiba bado

ni wizi kwa sababu alikuwa na nia hiyo . *Burglary* ni wizi wa usiku kuanzia saa 6:30 jioni hadi 6:30 asubuhi. Katika lugha ya Kiswahili hatuna dhana hizi mbili. Kwa sababu ya kutotofautisha dhana hizi katika Kiswahili haki inaweza kukiukwa. Ikumbukwe hukumu ya maovu haya mawili ni tofauti.

4.3.6 Jurisdiction

Wakalimani walitoa maana ya neno hili kama uwezo wa korti, mamlaka, enye nguvu, eneo ambapo kitendo kilifanyika, mamlaka ya sheria, au utekelezaji wa sheria. Neno hili moja lilionekana kuwa na tafsiri mbalimbali kulingana ni kwa muktadha upi lilitumika. Maana ya uwezo au enye nguvu na enye mamlaka ambayo ikitafsiriwa kwa kiingereza itakuwa power and authority haiwezi ikawa kisawe cha "*jurisdiction*". Cha muhimu kuelewa ni kuwa korti ina mamlaka ya kusikiza kesi kulingana na thamani fulani ambayo mdaiwa anadai au kutoka eneo fulani ambapo uhalifu utatekelezwa. Kwa mshtakiwa hata iwapo anaishi mbali na mahali ambapo ametekeleza uovu atashtakiwa kwenye korti ilio karibu na mahali alipotekeleze uovu ule. Hivyo basi, huu ni wajibu wa korti kujua ni wapi kesi hiyo itafanywa.

4.3.7 Cross-examination

Wafasiri walitoa tafsiri ya neno hili kama "*kuuliza maswali*". Hii hutokea baada ya ushahidi kutolewa. Mshtakiwa anastahili kuuliza maswali yanayomsaidia katika kesi hiyo. Washtakiwa wengi walieleza matukio yaliyotokea badala ya kuuliza maswali yanayotokana na ushahidi. Wengine kwa kutojua huuliza maswali yasiohusiana na kesi au wengine husema hawana maswali. Kwa wakati huu wanahitajika kuuliza maswali yatakayodunisha ushahidi uliotolewa ili usikubalike.

4. 3.8 Robbery with violence

Dhana hii ilitafsiriwa kama *wizi wa mabavu*. Ni vigumu kwa mtu wa kawaida kujua wizi wa mabavu. Labda neno hili lingeeleweka vyema kama ingelikuwa wizi wa kutumia nguvu. Tafsiri hii bado italeta utata kwa sababu 'robbery' ni 'unyang'anyi' na 'armed robbery' ni unyang'anyi kwa kutumia silaha. Isitoshe, hata ambapo wizi huo uliotendwa unahusu 'ujeuri' na 'juhudi' mbali na kuwa wa 'nguvu na ukali' bado fasiri waliyotoa ilikuwa ni 'wizi kwa kutumia nguvu au mabavu'. Pia dhana ili fasiriwa kama 'fujo' au hata 'mauaji' maelezo yaliyotolewa ni kwamba

hata iwe 'nguvu' hazikutumika; washukiwa wangefumaniwa na wenye mali au yeyote , fujo na hata mauaji yangetokea.

4.3.9 Confessions

Dhana hii ilitafsiriwa kama *kukiri, kukubali makosa, tubu au ungama.* Dhana hii inaleta utata kiasi kwamba mshtakiwa ni lazima akiri makosa. Ukweli ni kuwa anaweza kukiri kwa kukataa kwamba hakufanya kosa iwapo ana sababu zilizo na mashiko. Dhana 'tubu' au 'ungama' hizi katika lugha ya Kiswahili zinaweza kuchukulia katika dhana ya dini pale ambapo unapokubali makosa utasemehewa. Katika sajili ya sheria ukikiri makosa bado adhabu itatolewa.

.

4.3.10 Indecent assault

Neno hili lilifasiriwa kama *kupapasapapasa, uvamizi, shambulio ya nguvu, mapigo, najisi.* Wafasiri walieleza kuwa neno hili hutoa maana mbalimbali. Maneno, vishazi na virai vinapotumiwa inafaa ihakikishwe kuwa kunadhihirika yanayonuiwa matumizi yao ili kuhakikisha matumizi hayo yameimarika inavyohitajika.

Dhana hizi kwa namna zilivyotafsiriwa tofauti zinaonyesha kuwa maana iliotumika ilikuwa tofauti na hivyo ilipotosha. Isitoshe wakalimani walitoa maana tofauti katika dhana moja kuonyesha kuwa pia maana iliokusudiwa pia ingekuwa zaidi ya moja. Isitoshe katika kubainisha matatizo ya tafsiri na ufasiri jinsi wasailiwa walivyotoa maana tofauti katika dhana moja ilionyesha kuwa katika maongezi ya kawaida siyo lazima matumizi ya maneno yawe na maana mahsusi ilivyo katika sheria.

Saville-Troike (1989) anabainisha kwamba, maana katika matumizi rasmi ya lugha mahakamani ni mfumo unaotazamiwa kuwa wa wazi kwa wasemaji wa jamii fulani. Hii ni kwa sababu wasemaji ni wa utamaduni na mila inayotawaliwa na lugha inayoeleweka kwao. Uteuzi wa kimaana unatazamiwa kuakisi maarifa ya kijamii juu ya mazingira yao, kumbukumbu zao, historia yao na mawazo yao. Haya ndiyo hudhihirisha lugha inavyoishi katika bongo na ndimi wanaotumia lugh hiyo.

Kwa ajili ya upekee na umahsusi wa sajili ya kisheria, tunapata kwamba vizuizi vinavyotokana na kanuni za kisheria mara nyingi huwa umbomaana na matumizi yake huonekana katika matukio maalum. Hii ndiyo hali inayoonekana mahakamani. Kanuni za

kisheria huathiri hata wasomi wa nyanja zingine. Sajili ya sheria inawalenga wanasheria na hukusudiwa kufasiriwa makundi mengine inapohitaji.

Sentensi za matini huwa ndefundefu. Inawezekana kupata aya nzima ikiwa na umbo la sentensi moja tu. Sentensi hizi huwa ngumu kusomeka na kueleweka. Sentensi ndefu humfanya msomaji kupata ugumu wa kuhifadhi mambo katika hali ya mtiririko. Sentensi ya hakimu ikiwa ndefu itakuwa vigumu kwa mkalimani kuifasili. Hii ni kwa sababu hakuna muda wa kutosha kutulia na kutafakari anavyoweza kuendelea kutoa ufafanuzi wake.

Sajili ya kisheria hubainika kwa kuwa na msamiati na istilahi teule. Hutumia msamiati kama vile 'ndugu msomi', 'mheshimiwa' maneno haya huonyesha heshima. Nahau hizi hutoa maana maalum ambazo hazilingani na jumla za maana za maneno yaliyo katika tungo za matumizi ya lugha ya kawaida.

Kutumia msamiati maalum katika kuwasilisha hoja katika mahakama huleta matatizo hasa ufasiri unapofanywa. Baadhi ya matatizo haya ni kukosa kisawe kwa istilahi maalum za sajili ya sheria, inakuwa vigumu vilevile kwa mhusika asiye mwanasheria kuelezea baadhi ya msamiati au istilahi kwa kukosa ujuzi, elimu na mazoea ya matumizi yao.

4.4 Maoni ya hadhira kuhusu tafsiri

Sehemu hii inaelezea maoni ya hadhira waliohudhuria vikao katika mahakama. Mhusika mmoja kati ya waliohudhuria mashauri ya mahakama alichaguliwa. Huyu ni yule aliyeelewa lugha ya Kiswahili na Kiingereza. Alichaguliwa kimaksuudi. Idadi ya hadhira ya watu 9 walihojiwa. Kiambatanisho B uk. 68 kilitumika kukusanya maoni kutoka kwa baadhi ya watu waliohudhuria mahakama. Hadhira ilikuwa ni muhimu ili mtafiti asiegemee upande mmoja. Isitoshe wao pia walikuwa kama wachunguzi ili watathmini ukalimani unaofanyika na pia wao walichukuliwa kama kigezo cha kupima iwapo mawasiliano yanaenda sambamba. Washtakiwa hawangeweza kuhojiwa kwa sababu baada ya ushahidi wengine walirudishwa katika rumande au hawangetaka kuhojiwa.

4.4.1 Maoni ya hadhira jinsi ukalimani ulivyofanywa

Walitathmini ubora au udhaifu wa ukalimani kwa kutoa maoni mbalimbali kama inavyoonyeshwa katika jedwali 11.

Jedwali 11: Maoni ya hadhira jinsi ukalimani ulivyofanywa

Ukalimani ulifanywaje	Idadi	Asilimia %
Vizuri	2	22.22
Wastani	2	22.22
Haukueleweka	3	33.34
Haukuwa wa haki	2	22.22
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Jedwali hili linaashiria kuwa zaidi 50% inaonyesha kuwa ukalimani ulikuwa na shida kwa sababu aidha haukueleweka au haukuwa wa haki kwa sababu uliegemea upande mmoja wa LC au LL. Asilimia 22.22 ya hadhira walisema ukalimani ulifanywa vizuri. 22.22% ilipendekeza kuwa ukalimani ulifanywa wastani hapa walimaanisha kuwa mkalimani alitafsiri kwa kiwango cha kadiri hakuegemea upande wowote. Takwimu hizi hata hivyo zilizingatia maoni ya hadhira ya mtu mmoja ambapo ilichukuliwa kuwa aliwakilisha maoni ya wengine.

Kwa maoni ya hadhira, sehemu ambazo hazikueleweka vyema ni pale ambapo istilahi zilizotumika zilikuwa za sheria na hivyo waliona kuwa hazikueleweka vyema jinsi zilivyotafsiriwa. Isitoshe, ili kufasiri dhana za kitamaduni mfasiri alihitajika kupata visawe vya kitamaduni jambo ambalo lilionekana kuwa tatizo. Ukosefu wa visawe hivi ulifanya sehemu zingine zisieleweke. Ukosefu wa visawe ulibainika katika misemo au nahau ambapo hutumiwa kwa kufungamana na utamaduni wa watu fulani. Uchoraji wa dhana zinazowakilishwa na mafungu haya ya maneno sio tu hufanywa kwa usanii bali pia kwa kuzingatia desturi, imani, historia, mazingira na falsafa ya watumiaji wa lugha inayohusika. Hali hii ilifanya mafungu ya maneno ya namna hii yaweza kuwa magumu mno kufasirika katika lugha nyingine. Mfano neno "kuchapa maji" litamaanisha kupiga maji katika Kiingereza iwapo litatafsiriwa neno kwa neno kama "beating water". Katika jamii ya Waswahili neno hili humaanisha kunywa pombe ambayo ni lugha ya tafsida. Hadhira pia ilitoa wazo kuwa pia sehemu zingine hazikueleweka vyema kwa sababu ya wahusika kuongea kwa sauti hafifu, kuongeza yale ambayo hayakusemwa au

kudondosha yaliyosemwa. Jambo hili lilikuwa muhimu kuzingatiwa kwa kina kwa sababu hakimu alizingatia ushahidi jinsi ulivyofasiriwa

4.4.2 Maoni ya hadhira kuhusu maamuzi yanayofanywa na hakimu

Hadhira ilitoa maoni yao kuhusu jinsi hakimu hutoa maamuzi yake akizingatia kwamba ukalimini umefanywa. Hadhira ilitoa maoni kama hakimu katika kutoa hukumu yake aliegemea lugha chanzi au lugha lengwa. Matokeo yaliwekwa katika jedwali 12

Jedwali 12: Maoni ya hadhira kuhusu maamuzi yanayofanywa na hakimu

Hakimu alizingatia matamko yapi	Idadi	Asilimia %
Aliegemea lugha chanzi	6	66.67
Aliegemea lugha lengwa	3	33.33
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Maoni ya hadhira yalionyesha kuwa hakimu alizingatia habari zilizokuwa katika lugha chanzi kwa asilimia 66.67 na akizingatia lugha lengwa kwa asilimia 33.33. Hii ilionyesha kuwa kila kinachofasiriwa ni muhimu sana hivyo basi ni muhimu kuhifadhi ujumbe jinsi ulivyo katika LC. Ujumbe usipotoke.

4.4.3 Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikutafsiriwa vizuri

Hadhira ilitoa maoni iwapo kuna sehemu walitambua hazikutafsiriwa vyema. Maoni yao yaliwekwa katika jedwali 13.

Jedwali 13: Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikutafsiriwa vizuri

sehemu ambazo hazikufasiriwa vizuri	Idadi	Asilimia %
Ndiyo	6	66.67
La	3	33.33
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Asilimia 66.67 ya hadhira ilikiri kuwa kuna sehemu ambazo hazikutafsiriwa vizuri. Asilimia 33.33 ilisema tafsiri zilifanywa vyema. Hadhira iliamini kuwa baadhi ya mambo yaliyo katika LC yalidondoshwa yalipofasiriwa. Isitoshe, baadhi ya matamko yaliongezwa, baadhi ya maneno yalikwepwa.

4.4.4 Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikueleweka

Hatimaye wahojiwa walitakiwa kujibu iwapo kuna sehemu ambazo hawakuzielewa. Walihitaji kujibu 'ndiyo' au la. Majibu yao yalidhihirishwa katika jedwali 14

Jedwali 14: Maoni kuhusu sehemu ambazo hazikueleweka

Sehemu ambazo hazieleweki	Idadi	Asilimia %
Ndiyo	7	77.78
La	2	22.22
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Asilimia 77.78 ya wahojiwa walikiri kuwa kuna sehemu ambazo hazikueleweka vyema na asilimia 22.22 ilikiri kuwa sehemu zilieleweka vyema. Sababu walizotoa ilikuwa ni kwamba hawakuelewa istilahi au lugha ya sheria iliyotumiwa ama baadhi ya maneno ambayo hayakutafsiriwa. Isitoshe, tofauti katika tamaduni za lugha hizi zilitambuliwa kama sababu za kufanya sehemu hizo kukosa kueleweka.

4.5 Uchanganuzi wa matamko yaliyokalimaniwa

Matamko yaliyokalimaniwa yalikuwa na umuhimu mkubwa katika kuchangia deta. Kwa kuchanganua kwa kina sehemu ambazo zilikuwa na makosa zilitambuliwa. Hii ilikuwa njia ya kupata deta halisi ya kilichokuwa kikitendeka mahakamani. Aidha, mtafiti aliandama njia hii kwa kuzingatia ufafanuzi wa watafiti wengine kama vile Best na Khan (2000) kuwa deta iliyokusanywa katika hali hii huwa asili na isiyoathiriwa na maelezo ya watu wengine kama vile ilivyo katika deta ya mahojiano na hojaji. Rejelea kiambatisho C. uk. 69 -79.

4.5.1 Muhtasari wa matamko yaliyonaswa, tarehe, saa, nambari ya kesi na ilihusu nini

Jedwali 15 ni muhtasari wa matamko yaliyorekodiwa katika kikao cha 1-9 (C1-C9) uk70-79. Pia tarehe ambapo kesi hiyo ilifanyika, saa ambapo kesi hiyo ilifanywa, nambari ya kesi na kesi ilihusu nini.

Jedwali 15: Muhtasari wa matamko yaliyonaswa, tarehe, saa, nambari ya kesi na ilihusu nini


Matamko	Tarehe	Saa	Nambari ya kesi	Kesi ilihusu nini
C1	2/3/2011	9:04 Asubuhi	793/2010	Wizi wa ng'ombe
C2	3/3/2011	10:55 Asubuhi	2702/2007	Mauaji
C3	7/3/2011	4:23 Jioni	449/2011	Wizi
C4	9/3/2011	9:30 Asubuhi	68/ 2011	Ubakaji
C5	16/3/2011	11:45 Asubuhi	1835/2010	Misokoto ya bangi
C6	24/3/2011	4:04 Jioni	443/2011	Vita
C7	6/4/2011	3:12 Jioni	861/2010	Ajali barabarani
C8	14/4/2011	9.32 Asubuhi	917/2011	Kuwa na silaha kinyume na sheria
C9	26/4/2011	11:24 Asubuhi	2590/2010	Shamba

Asili: Matokeo ya utafiti

4.6 Maelezo ya matatizo ya tafsiri na ufasiri

Kwa kurejelea kiambatanisho C uk.69-79 kilichohusu matamko yaliyokuwa yamenaswa, uchanganuzi wa kina ulifanywa. Muhtasari wa matatizo yaliyotambuliwa yaliwekwa katika jedwali 16

Jedwali 16: Muhtasari wa matatizo ya tafsiri na ufasiri



Asili: Matokeo ya utafiti

Kutokana na uchanganuzi wa matamko mtafiti alibaini kuwa kulikuwa na makosa 64 katika matamko yaliyonaswa. Makosa ya utamaduni yalikuwa 18 yakiwakilisha 28.11% ya makosa yote. Makosa ya udondoshaji yalikuwa 15 yakiwakilisha 23.44 %, makosa ya nyongeza 14, ikiwa ni 21.88%, ujumbe uliopotoka makosa 11, ambapo ni 17.11% , na makosa anuwai 6 ambapo ni 9.38%. Mtafiti alitoa mifano michache katika kila kitengo cha makosa hayo.

4.6.1 Makosa yatokanayo na utamaduni

Mtafiti alichunguza matamko katika LL na LC kubainisha ni kwa njia ipi utamaduni huzua matatizo. Msamiati wa lugha hujenga maana za maneno kutokana na utamaduni wa jamii inamozungumzwa lugha hiyo. Hivyo, maana za maneno ni kiungo au daraja madhubuti kati ya utamaduni na lugha; na hicho ndicho kitovu cha ukalimani. Kiambatisho C 4.3 uk.73 kinaonyesha jinsi utamaduni huzua matatizo. Tazama mfano.

Nukuu a

AC: No your honour, I didn't touch her I just touched the ***upper part and the lower part.***

IN: Alimgusa sehemu ya juu na chini tu

Kiambatisho C4.3

Mshtakiwa katika ile hali ya kuficha aibu anatumia neno "I never touched her, I just touched the upper part and the lower part". Vilevile

Nukuu b

CO: Lakini si wewe ***huchapa maji.***

kiambatisho C7.4

"***Kuchapa maji***" kinaashiria kitendo cha kulewa. Jambo hili ni muhimu na linathibitisha nadharia tete kwamba kuna matatizo masuala ya utamaduni yasipozingatiwa. Isitoshe, (Moeketsi na Swanepoel, 1997) wanasema kwamba matatizo ya ukalimani yanachangiwa na utamaduni jinsi watu hutumia lugha yao hasa katika maneno ya mwiko ambayo hayawezi kutajwa kama vile sehemu za siri, vitendo vya ngono na taka mwili. Hivyo basi, matumizi ya tasfida yaweza kupoteza maana ya ujumbe kama ilivyobainika katika utafiti uliofanywa miongoni mwa jamii ya Basotho kule Afrika kusini pamoja na jamii nyingi za Kiafrika. Matumizi ya tasfida katika mahakama yaliathiri ushahidi. Ikumbukwe kuwa kile kinachosemwa na lugha inavyotumiwa ni muhimu sana. Kwa mfano, katika jamii hii badala ya kusema "urinate" walitoa dhana ya "pass water" hivyo kubadilisha ujumbe

Ili kufasiri matini zenye dhana za kitamaduni mfasiri anayetumia lugha za Kiingereza na Kiswahili alihitajika kupata 'visawe vya kitamaduni' vilivyo mwafaka katika lugha anazozifanyia kazi. Visawe hivyo visipopatikana, basi mfasiri alipata matatizo makubwa. Mtafiti alibainisha kuwa mkalimani alikumbana na visawe ambavyo ilibidi vitumike jinsi vilivyo katika kiingereza kwa mfano:

Nukuu c

IN:Wapi nyundo kama ***exhibit***

kiambatisho C 6.5

Neno exhibit lilibaki vivyo hivyo baada ya fasiri. Pia neno ***jam*** lilibaki vivyo hivyo. Mfano.

Nukuu d

Ac: How did you know that I was driving reckless when there was jam?

IN: Ulijuaje niliendesha gari vibaya na kulikuwa na ***jam****?*

Kiambatisho C 7.10

Wakati mwingine kwa kukosa visawe aliweza kuhamisha kwenye uzungumzi au LL ufafanuzi wa dhana hiyo inayohusika. Pia aliweza kufanya ukopaji wa maneno au utohozi kwa mfano bondi kutokana na neno "bond"

Nukuu e

MA: *You have been given* ***a bond*** *of five hundred thousand shillings or something of equal Value to that money.*

IN: *Utoe* ***bondi*** *ya shilingi elfu mia tano au thamani ya kitu kinachotoshana na pesa hizo.*

Kiambatisho C 8.5

Tofauti za kimazingira zilileta matatizo katika kuyapata maneno yanayofanana au yanayowasilisha dhana moja. Matatizo mengi yalizuka tunaposhirikisha tamaduni mbili katika ukalimani. Baadhi ya matatizo ni: Kukalimani kijuujuu, kuyahepa baadhi ya maneno, kutopata uwiano halisi kwa sababu ya tofauti za kimazingira, utamaduni wa vifaa, wa kijamii na wa lugha. Hii inadhihirika waziwazi katika kiambatisho cha C4.1

Nukuu f

WI: on observation, the patient's ***vagina*** *and* ***vulva*** *were swollen and bruised.The* ***hymen*** *was also broken. This was enough evidence that somebody had a carnal knowledge of her that involved* ***actual penetration.***
IN: Daktari alipomkagua alipata ushahidi kuwa ulimfanyia ***kitendo hicho.***

kiambatisho cha C4.1

Mfasiri kwa sababu ya ukosefu wa visawe vya ***vagina, vulva, hymen, actual penetration*** anakwepa yote na kusema ***ulitenda kitendo hicho***. Hii inapotosha kwa sababu kitendo sio kimoja tu.

Ilibainika kuwa ukalimani siyo tu mchakato wa kiisimu bali pia ni mchakato unaojumuisha masuala yanayohusu utamaduni. Ili kufasiri dhana za kitamaduni mkalimani anawajibika kuelewa tamaduni za lugha zote mbili anazozishughulikia. Ni vigumu kujua mnenaji alinuia kusema nini ikiwa hautaelewa utamaduni wa lugha anayotumia. Ukosefu wa uelewa huu uliweza kusababisha matatizo katika ujumbe wa LL. Nida (1964) na Mwansoko (1996) wote wanaafikiana kuwa matatizo mengi ya tafsiri ni ya kitamaduni na kimazingira ambayo hutokana na kutopata visawe kwa sababu ya tofauti katika utamaduni wa jamii, utamaduni wa vifaa,

utamaduni wa dini na utamaduni wa lugha. Mazingira au ekolojia pia ni sehemu ya utamaduni. Hivyo basi, ni vigumu kujua mnenaji alinuia kusema nini ikiwa hautaelewa utamaduni wa lugha anayotumia. Katika matokeo yetu pia makosa ya utamaduni na kimazingira ndio yaliyokuwa mengi.

4.6.2 Makosa ya udondoshaji

Makosa ya udondoshaji yalitokea wakati baadhi ya maneno, virai, vishazi, maoni, sentensi au sehemu ya matamko yaliachwa ukalimani ulipofanywa. Udondoshaji umejitokeza katika kiambatisho C.1 uk.70

Nukuu g

PR: Your honour, in this matter I wish to apply for an adjournment. My next witness who is the investigating officer, is not feeling well..

MA: Yes, when is he expected back?

(Baada ya mashauriano dakika 3)

PR: ***I have been informed he will be back in 3 days time, your honor.***

MA: Yes, any objection?

IN: Kiongozi wa kesi anaomba kesi ihairishwe kwa sababu yule shahidi alikuwa aitetea hayuko. Unakubali au unapinga?

(Baada ya kimya kirefu)

AC: Sielewi

IN: ***Unakubali au unapinga****? Hilo ndilo swali*

(kesi hii itasikizwa machi 9)

Kiambatisho C.1

Mazungumzo yanaendelezwa kati ya kiongozi wa mashtaka na hakimu. Afisa wa uchunguzi alihitajika aje atoe ushahidi lakini alikuwa mgonjwa. Ingawa hakimu anataka kujua atarudi lini mshtakiwa hajaelezwa katika tafsiri inayofanywa. Swala la muda ni muhimu sana katika sheria. Anapoulizwa kama anakubali kesi ihairishwe haelewi ni kwa njia ipi. Mfasiri hakutafsiri habari

yote. Mshtakiwa amewachwa au kutengwa katika mawasiliano. Haelewi kama anakubali makosa aliyofanya au kesi ihairishwe. Mkalimani amefanya ufupisho wa habari na hivyo kuwacha habari muhimu kama afisa wa uchunguzi atapatikana baada ya siku tatu.

Vilevile Kiambatisho C.2 uk. 71 kinaonyesha udondoshaji

Nukuu h

MA: Just a minute, who are the witnesses in this case?

PR: There are three more, your honour... the two girls are the complainants of the doctor and the investigating officer... They are four, your honour.

MA: Have you checked on P3 forms...the doctor's conclusion?
PR: Your honour. I have not had time to....

MA: Isn"t that not a file.

PR: Y es...

MA: What does it say? any evidence brought before it'...
PR: Y es. Your honour.
MA: Will doctor's evidence and the investigating officer help us...

PR: Y es, it seems ...but we need more clarification may be girls...

MA: How old are the girls... the victim
PR: They are — both of them are 8 years old, your honour.

MA: Are there no adult witness? a person who may be saw the accused with the girls? You know ... because the only real evidence you have is what the girls will say... There is no way the court will convict somebody on the basis of the testimony of eight-year olds about something that happened over two month ago. Do you get what I am saying? .

PR: Yes. Your honour, I think I will link with

the investigating officer to find out if there are other witnesses so that...

MA: You will know what to do for now. Let's take a hearing date. Eh...9th March?

PR: Most obliged your honour.

IN: ***kesi yako itasikizwa tarehe 9 machi***

(Your case will be heard on 9th March.)
Kiambatisho C.2

Kuna udondoshaji wa habari au ujumbe ambapo mshtakiwa ametengwa katika mawasiliano. Mawasiliano kati ya kiongozi wa mashtaka na hakimu ambapo kesi haiwezi kuendelea kwa sababu ushahidi unaotolewa hauna mashiko. Inabidi kesi ihairishwe. Mjadala huu mrefu unatokea katika kutatua suluhisho kati ya hakimu na kiongozi wa mashtaka. Mshtakiwa anaelezwa tu kesi yake itasikizwa tarehe 9 machi bila kuelezwa ni kwa nini.

Katika kiambatisho C 4.1 uk. 73 kuna udondoshaji

Nukuu i

WI: ***on observation, the patient's vagina and vulva were swollen and bruised. The hymen was also broken. This was enough evidence that somebody had had carnal knowledge of her that involved actual penetration.***
IN: ***Daktari alipomkagua alipata ushahidi kuwa ulimfanyia kitendo hicho.***
Kiambatisho C 4.1

Daktari anayetoa ushahidi anasema kuwa sehemu za siri za mlalamishi zilikuwa zimejeruhiwa na kuvimba na pia ubikira ulikuwa umetobolewa jambo lililoonyesha kuwa mshtakiwa alikuwa amembaka. Katika kufasiri mkalimani anatoa muhtasari kwa kusema kuwa mshtakiwa alifanya kitendo hicho. Anawacha habari au maelezo muhimu yanayotolewa na daktari.

Kiambatisho C 8 uk. 78, kinaonyesha makosa ya udondoshaji.

Nukuu j
MA: You are charged with possession of ***A.K 47 gun with 5 rounds of Ammunition.****Do you plead guilty or not*
IN: ***unakubali mashtaka au unakataa***
Kiambatisho C 8

Kiongozi wa mashtaka anasoma mashtaka lakini mkalimani hatafsiri mashtaka yenyewe bali anauliza kama mshtakiwa anakiri mashtaka yenyewe. Sehemu muhimu kama kuwa na bunduki AK 47 na risasi 5 inawaachwa bila kutafsiriwa vilevile katika C 8.9 uk. 78 neno ***tittle deed na caution*** imedondoshwa na mshtakiwa anaelezwa aje na barua.

Nukuu k

ACCUSED: Ndio watu wa jamii wako hapa.
[Akielekeze kidole kwa aliyesimama)

MA: [Addressing the person who has stood up]

> *(If it is* ***a title deed*** *you want to bring, you take it first for a valuation to be done, that piece of land to be seen is of what value. The* ***caution*** *you will be given when the valuation is done come with it together with the tittle deed. Do you understand?)*

IN: ***Nadhani*** *umeelewa ulete* ***barua***
Kiambatisho C 8.9

Mkalimani anasema kuwa anadhani ameelewa ilhali hajatafsiri sehemu nyingine. Gonzalez (1991) anasema kwamba ujumbe ukiachwa au ukidondoshwa wanaofasiriwa hawataelewa ambapo inaweza kuleta shauku au kutoafikiana ama kumfanya mmoja ajihisi hajahusishwa katika kesi ipasavyo. Jambo hili ni muhimu sana kwa sababu lengo kuu la shughuli za mahakama ni kuhakisha mshtakiwa anahusishwa katika kufuata yanayoendelea katika mahakama. Iwapo mkalimani atafanya muhtasari wa matamko ataweza kuwacha habari muhimu. Kukosa kutambua uwepo wa mshtakiwa ni kumnyima haki yake. Mshtakiwa ni vyema aelezwe yote yanayoendelea.

4.6.3 Makosa ya nyongeza

Makosa ya nyongeza ya ujumbe yalijitokeza ambapo sehemu ambazo hazikuwa katika LC ziliongezwa katika LL. Kiambatisho C 1.4 uk. 70 ni mfano wa jinsi nyongeza imetumika.

Nukuu l
MA: Yes, any ***objection?***
IN: ***Kiongozi wa kesi anaomba kesi ihairishwe kwa sababu yule shahidi alikuwa aitetee hayuko****. Unakubali au unapinga?*
Kiambatisho C1.4

Hakimu anatumia neno **objection** neno hilo linatafsiriwa kama ***unakubali au unapiga***. Badala yake anatoa maelezo kabla hajalitafsiri.

Nukuu m

MA: ***Mitigation****?*
IN: Malilio.
*AC: Eh...*ndio mheshimiwa.

IN: ***Kuna kitu ungetaka kuambia mahakama kabla hujahukumiwa?... Hii sio saa za kuelezea vile ilikuwa... Si ulitoa ushahidi wako?***

Umepatikana na hatia na sasa inatakikana useme kama una shida yoyote korti inaweza kuangalia kabla haujahukumiwa Eeh ... useme vitu kama ... watoto... bibi ... kama uko na ugonjwa fulani, wanaokutegemea...kazi...

Kiambatisho C5

Hakimu anasema ***mitigation*** lakini kwa sababu mshtakiwa haelewi mfasiri anaendelea kufafanua zaidi. Mfasiri anatoa fununu kwa mshtakiwa iwapo ana shida aeleze mahakama. Anamwelekeza zaidi kwa kumtajia mambo anayohitaji kutaja kama iwapo ana watoto, bibi, ugonjwa au wanaomtegemea

Pia, kiambatisho C 6.9 uk. 76 kinaashiria kosa la nyongeza katika ukalimani

Nukuu n

MA: Lack of evidence... Lets take another hearing date...16th

IN: Kesi hii imehairishwa kwa sababu ya ***ushahidi ambao si kamili.***

kiambatisho C 6.9

Hakimu anamweleza mshtakiwa kwamba kesi imehairishwa kwa sababu ya kukosa ushahidi. Mkalimani anapotafsiri anaongeza neno **ushahidi kamili**. Hii ni kwa sababu anajua kwamba labda atauliza ni kwa nini. Mkalimani kwa sababu ya tajriba anajua moja kwa moja shughuli za mahakama hazitaendelea mbele kwa sababu ametaja kuwa hana mashahidi. Kuahirisha kesi ni kutoa fursa kwa mashahidi wote watoe ushahidi.

Kiambatisho C 9.2 uk. 79 neno ***defense*** limefafanuliwa ili mshtakiwa aelewe zaidi.

Nukuu o

PR: Leo ikiwa ni siku ya kusikiza kesi yako unashtakiwa kwa kuuza shamba ya ekari 10 kwa wanunuzi wawili Kwa wakati mmoja.

MA: ***Defense.***

IN: Sasa ni wakati wako wa kujitetea.
Na kuna njia tatu za kujitetea. *Unaweza kujitetea ukiwa hapo ambapo hautaapishwa na hautaulizwa maswali. Kama uko na mashahidi unaweza kuwaita.*

Njia ya pili unaweza kuja upande huu ambapo utaapishwa na utaulizwa maswali. Kama uko na mashahidi unaweza kuwaita.

Njia ya tatu, unaweza kuamua kukaa kimya na uongenjee uamuzi wa mahakama.

Kiambatisho C 9.2

Neno hilo ***defence*** linaangaziwa kwa kutoa njia tatu ambazo mshtakiwa anaweza kujitetea. Nyongesa hii ndefu yaweza kumwelekeza mshtakiwa

4.6.4 Maana potovu

Tofauti za maumbo, miundo na maana kati ya Kiswahili na Kiingereza husababisha upungufu katika ukalimani hii huzua maana potovu. Kwa mfano, Kiambatisho C 6 uk. 76

Nukuu p

AC: I beat him with 3 blows of hammer

IN: Alimpiga ***na nyundo tatu****.*

Kiambatisho C 6

Mshtakiwa alimaanisha kuwa kuwa alitumia nyundo moja lakini akampiga mara tatu. Hii ni kinyume anavyotafsiri mkalimani kuwa alimpiga na nyundo tatu.

Maumbo ya Kiingereza kwa mfano, huruhusu kauli nyingi elekezi kutoonyesha umoja au wingi wa wahusika, wakati wala majina ya vitu mahususi vinavyoambatana na maelekezo yanayotolewa. Hivyo mfumo huu wa maumbo huwezesha kutoa taarifa zilizopana zaidi. Kwa upande mwingine, mfumo wa Kiswahili hulazimu kubainisha vipengee vyote. Kwa mfano, ili kufanikisha mawasiliano mtu anayekalimani kutoka lugha moja hadi nyingine wakati mwingine hulazimika kutumia kirai katika LL kuwasilisha dhana ambayo katika LC ni neno moja tu. Mfano kiambatisho C 4.1 uk. 73

Nukuu q

WI: On observation, the patient's vagina and vulva were swollen and bruised.The hymen was also broken. This was enough evidence that somebody had had carnal knowledge of her that involved actual penetration.

IN: Daktari alipomkagua alipata ushahidi kuwa ulimfanyia kitendo hicho.
MA: Did you have ***carnal knowledge*** *of the complainant?*

IN: Je ulimnajisi mshukiwa? (Did you rape her?)

Kiambatisho C4.1

Kwa sababu ya kukosa kisawe mwafaka, dhana **carnal *knowledge*** lilitafsiriwa kama kumnajisi. Fasiri hii inapotosha. Dhana carnal knowledge lina maana pana kutegemea muktadha au hali.

Grice (1975) anapendekeza kaida ya ushirikiano katika jitihada za kuelezea jinsi maana ya mzungumzaji huzuka. Kaida ya ushirikiano inasema kwamba "zungumza kama inavyostahili; mahali panapostahili kwa nia inayokubalika na mwelekeo wa mazungumzo ambapo wewe unahusika (Thomas, 1995) Kaida hii ya ushirikiano hubeba kanuni nne:

1. Kiasi: Hakikisha habari unayotoa inafahamisha kama vile inavyostahili. Usitoe habari inayofahamisha zaidi ya vile inavyostahili.
2. Thamani: Usiseme yale unayoamini kuwa uongo. Usiseme yale ambayo hauna ithibati ya kutosha
3. Uhusiano: Zungumza yale tu yanayohusiana na mada.
4. Namna: Jiepushe na utani unaoweza kukufanya usieleweke kwa kujiepusha na Utata. Tumia maelezo mafupi kwa mpangilio maalumu.

Kanuni hizi zinaelekeza yale yanayopaswa kufanywa na mshiriki ili wazungumze kwa njia inayoeleweka kwa urahisi. Wanapaswa kuzungumza ukweli, kuzingatia mada iliopo huku wakitoa habari kamili. Maoni ya Grice yalikuwa ni muhimu katika utafiti kwa sababu mkalimani ni lazima achanganue maana mbalimbali za matamko kama yalivyojitokeza ukalimani ulipofanywa kortini.

4.6.5 Makosa anuwai

Haya ni makosa ambayo mtafiti alihisi kwamba yalitatiza mawasiliano lakini hayakuzingatiwa katika makundi makuu. Makosa haya yalitokana na athari za kuchanganya msimbo au misimu.

Kiambatisho C 4.11 uk. 73 ***unisave unipe huku chini*** iliashiria kuomba wafanye mapenzi.

Nukuu r

AC: No, we agreed and she gave me.

CO: La sikukubali aliniambia ***nimsave nimpe huku chini*** *jambo nililokataa*
Kiambatisho C4.11

Kiambatisho C 6.3 Dhana ***nilihustle***. Ilidhamiria kutoa maana alijitahidi

Nukuu s
CO: ***Nilihustle*** *naye mpaka nikabaki na nyundo ambayo nataka kuitoa kama Ushahidi. (I managed to struggle with him till I retained the hammer which I intend to use it as exhibit).*
kiambatisho C 6.3

4.7 Kubainisha kiini / chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri

Sehemu hii inaelezea matatizo yaliyotambuliwa katika matamko. Katika sehemu hii tulionyesha jinsi mfasiri alivyotekeleza tafsiri na ufasiri kwa kutazama wajibu au majukumu yake. Katika sehemu hii tulitazama ni nini asili ya matatizo haya.

4.7.1 Ufahamu wa majukumu/ wajibu wa mkalimani

Matamko yaliyochanganuliwa yalimsaidia mtafiti kutambua iwapo alielewa wajibu wake. Mtafiti alibainisha kuwa ufahamu wa majukumu au wajibu ulichangia katika matatizo ya ufasiri. Matokeo yaliwekwa katika jedwali 17.

Jedwali linaonyesha kuwa katika ufasiri kutokana na matamko, wakalimani walitekeleza majukumu kadha wa kadha. Asilimia 55.56 ilikuwa ni kuratibu na kufasiri, asilimia 22.22 ilionyesha kuwa mkalimani alifanya tafsiri ya neno kwa neno. Isitoshe, asilimia 22.22 ilidhihirisha kuwa mkalimani alitafsiri huku akimsaidia mshtaki au mshtakiwa.

Jedwali 17: Muhtasari wa matamko kuhusu ufahamu wa majukumu / wajibu wa mkalimani

Jukumu /wajibu	**Idadi**	**Asilimia %**
Kuratibu na kufasiri	5	55.56
Kufasiri neno kwa neno	2	22.22
Kuwasaidia washtakiwa kuelewa matamko vizuri	2	22.22
Jumla	9	100

Asili: Matokeo ya utafiti

Mfasiri alitekeleza wajibu mkubwa katika kufanikisha mawasiliano. Matamko yaliyonaswa yalionyesha kuwa mfasiri alitekeleza majukumu mawili makuu kuratibu na kutafsiri. Tazama mfano huu.C3 uk. 72.

Nukuu t

CO: If I tell the court you were beaten up because you had developed a habit of visiting me when my husband is not there, would I be lying?

IN: Nikieleza mahakama kuwa ***ulikuwa umezoea kuja kwangu*** *usiku kila siku ukijua mume wangu hayuko nitakuwa nikidanganya?*

Kiambatisho C 3.1

Kiambatisho C 3 mfasiri anatumia lugha ya adabu. Anaondoa ukali wa maneno jinsi yalivyo huku akikwepa kuelezea mahakama kuwa mshtakiwa alipigwa kwa sababu ya mazoea ya kwenda kwa wenyewe usiku. Jambo hili linaoana na utafiti uliofanywa na (Seligson, 1999) ambaye alibainisha kuwa wafasiri hupunguza ukali katika maswali kwa kuuliza kwa njia yenye adabu. Hii ni kinyume na maadili ya kazi yao ingawa lengo lao ni kufanya mashahidi au washtakiwa wasiwe na hofu. Adabu hii pia, inajitokeza ambapo wakalimani wanatuima lugha ipasavyo. Kiwango chao cha lugha ni cha juu ikilinganishwa na mshtakiwa. Katika kiambatanisho C3 katika kutoa ushahidi wake anasema kuwa anayoelezea ni kweli na si uongo hayatiliwe maanani na kalimani. Maneno kama "nitakuwa nikidanganya" hayatiliwi maanani. Korti haina haja kujua kama utakuwa unadanganya kwa sababu inatarajia kuwa unaongea ukweli mtupu. Shlesinger (1991) anabainisha kuwa wafasiri hutaka kuonyesha kuwa wamebobea katika kukabiliana na udhaifu wowote unaoweza kukomesha mawasiliano ili mazungumzo kati ya mshtaki na mshtakiwa yasikatike. Gonzalez (1991) na Mikkelson (1998) wanapendekeza kuwa mkalimani atoe habari ilio sawa au ilingane na ile ilio katika LC bila kupoteza maana iliyokusudiwa. Vilevile atoe athari ya matamko sawa na ilio katika LC. Moeketsi (1999) anasema kuwa ili kufasiri ipasavyo ni lazima mkalimani aelewe wajibu wake ipasavyo kwa kujihadhari na kutoa maoni ya kisheria, kiisimu au kufungwa na utamaduni wake.

Isitoshe, Katika kiambatisho C3 uk. 72 inaelekea kuwa mkalimani anamwongoza mshtakiwa.

Nukuu u

IN: You...do you realize you are in court, you...
MA: What is his answer?
AC: Those are lies, your honour.
IN: ***Eleza mambo yanayohusiana na wizi wa televisheni.***
kiambatisho C 3

Mfasiri anamkumbusha mshtakiwa kuwa yuko kortini na anahitajika atumie lugha ya adabu. Tulitarajia mfasiri angelitafsiri yaliosemwa lakini hatekelezi wajibu wake badala yake anamwelekeza mshtakiwa aeleze mambo yanayohusiana na wizi wa televisheni. Tulitarajia mkalimani angelitekeleza haki na usawa kwa kutafsiri ujumbe jinsi ulivyo kutoka LC hadi LL bila kuegemea upande wowote.

Katika utafiti ilibainika kuwa baadhi ya wakalimani waliamini kuwa wajibu wa mkalimani ni kuwasaidia wale ambao hawaelewi Kiingereza kuwafanikisha kushinda kesi. Hili ni jambo linalokiuka maadili ya kijamii na haki; kwa sababu wakalimani wa kitengo hiki walitoa ufafanuzi kinyume na jinsi ulivyo katika LC ili kuwawezesha wasioelewa /ongea Kiingereza kuelewa zaidi au wakati mwingine hufanya ukalimani unaowaelekeza kupata majibu jambo linalowafanya kushinda. Hapa mkalimani anachukua wajibu wa wakili ilhali twajua hahitajiki kuegemea upande wowote. Jambo hili linajitokeza katika kiambatanisho C 5.1 uk.74 baada ya ushahidi kutolewa na hukumu unataka kutolewa hakimu alisema neno "mitigation" au hutafsiriwa malilio. Mtafiti alitambua kuwa mfasiri alilifafanua zaidi neno hili na kumwelekeza mshtakiwa. Hii ni kwa sababu anachukulia kuwa mshtakiwa hujui aseme nini katika hatua hii. Tazama kiambatisho C 5.7 uk. 74-75

Nukuu v

IN: ***Eeh ... useme vitu kama hizo ... watoto... bibi ... kama uko na ugonjwa fulani, wanaokutegemea.***
kiambatisho C 5.7

Mfasiri anamwelekeza aseme kuhusu habari za watoto, bibi, ugonjwa au wanaomtegemea ili korti imhurumia katika kulegeza hukumu itakayotolewa. Katika Kiambatisho C4.3 uk. 73

Nukuu w

AC: No your honour, I didn't not touch her I just touched the upper part and the lower part

IN: ***Alimgusa sehemu ya juu tu na chini tu.***

Kiambatisho C4.3

Hii inaonyesha jinsi mfasiri anayokalimani neno kwa neno kama mashine bila kuzingatia maana ya ndani. Kazi yake ni kurudia au kusema yale yanayosemwa kwa lugha moja hadi nyingine. Msimamo huu unashikiliwa sana na wanasheria ingawa huzingatia kuwa ni lazima ujuzi wa lugha utiliwe maanani. Kazi ya mkalimani ni kufanya ukalimani wa matamko jinsi yanavyowasilishwa bila kujali kama yanaeleweka au kama maana iliokusudiwa imewasilishwa. Iwapo mkalimani atafanya ukalimani kama huu basi utakuwa na shida. Katika mahojiano, wakalimani walikiri kuwa lugha ya sheria ndio chanzo cha matatizo katika ukalimani wa kortini kwa sababu jinsi inavyotumika inabidi kutafsiri neno kwa neno hasa ushahidi unapotolewa na hivyo kupotosha maana. Katika mapendekezo yao, ili kufasiri ipasavyo ni lazima mkalimani aelewe wajibu wake ipasavyo kwa kujihadhari na kutoa maoni ya kisheria, kiisimu au kufungwa na utamaduni wake.

Chanzo cha matatizo ya ukalimani ni wale wanaokalimaniwa hii inajionyesha katika kiambatanisho C 1.5 na C 1.6 uk. 70.

Nukuu x

IN: Kiongozi wa kesi anaomba kesi ihairishwe kwa sababu yule shahidi alikuwa aitetea hayuko. Unakubali au unapinga?
(Baada ya kimya kirefu)
AC: ***Sielewi***

kiambatisho C 1

Mshtakiwa kwa sababu ya kutofuata yanayoendelea kortini au kwa sababu ya kukosa kuelewa lugha ya sheria anasema haelewi huku akitarajia kuwa mfasiri atamfafanulia zaidi. Mahojiano ya hadhira na wafasiri yalibainisha kuwa wanaokalimaniwa hasa wasioelewa LC pia huwa hawaelewi wajibu wa mkalimani na hivyo hutarajia kuwa mkalimani kazi yake ni kutoa mwongozo, mashauri au usaidizi. Pia wakalimani waliamini kuwa kazi yao ni kufanikisha mawasiliano. Baadhi yao waliwajibika kufanya marekebisho katika baadhi ya matamko ili kuboresha uelewaji au muwala ili ueleweke vyema. Hatua hii ilizua tatizo. Jambo hili ni kinyume na Taft, (1981) anayesema kuwa mkalimani hastahili kuegemea upande wowote. Vilevile, hisia zake hazistahili kumwongoza katika ukalimani. Anawajibika asiegemee upande wa LC wala LL

hivyo basi ni lazima afasiri ujumbe ipasavyo. Kwa upande mwingine, mtafiti alitambua kuwa mkalimani ana majukumu mawili muhimu mbali na kufasiri anahitajika pia kuratibu. Inapasa wakalimani katika nyanja ya uanasheria wawe waaminifu wanapofasiri ili kutoa tafsiri ya matamko ipasavyo.

SURA YA TANO

MUHTASARI, HITIMISHO NA MAPENDEKEZO

5.1 Utangulizi

Katika sura hii, mtafiti ameshughulikia muhtasari wa matokeo yaliyoibuka kutokana na madhumuni ya utafiti huu yaliyokuwa kutambulisha na kueleza matatizo ya tafsiri na ufasiri. Pia, kubainisha kiini / chanzo cha matatizo ya tafsiri na ufasiri. Pia, ametoa mchango wa utafiti huu. Vilevile, amegusia matatizo aliyokumbana nayo wakati wa utafiti. Isitoshe, ametoa mapendekezo jinsi ya kukabiliana na matatizo ya tafsiri na ufasiri. Tamati, amependekeza kuhusu sehemu zinazohitaji kufanyiwa utafiti zaidi.

5.2 Muhtasari wa matokeo

Sehemu hii inatoa muhtasari wa utafiti ikizingatia madhumuni ya utafiti kwa kutambua na kueleza matatizo ya nyongeza, udondoshaji, utamaduni, maana potovu na makosa anuwai. Pia, tulijadili sababu mbalimbali zilizosababisha makosa haya.

5.2.1 Kutambulisha na kueleza matatizo ya tafsiri na ufasiri

Ilibainika kuwa kulikuwa na matatizo mbalimbali katika ukalimani. Matatizo ya nyongeza yalitambuliwa. Haya yalitokea kwa kuongeza sehemu zingine ambazo hazikuwa katika LL. Mambo haya yalijitokeza wakati matamko mengine yalirefushwa hivyo kupotosha ujumbe asilia. Mambo kadha wa kadha yalionekana kuchangia.

Sajili ya sheria au mahakama hutumia msamiati ambao una urasmi mwingi huku baadhi ya istilahi ni za kilatini. Hili humfanya mfasiri kuchukulia kuwa mshtaki au mshtakiwa haelewi istilahi za sheria na hivyo hubidi afafanue zaidi kwa sababu yeye huelewa hatua ambazo hakimu huchukua kutokana na tajriba ili waelewane wao kwa wao ili asikatize mawasiliano badala ya kuhamisha ujumbe jinsi ulivyo. Katika kuchukua hatua hii, mfasiri hutawala au hutoa uamuzi wake. Hapa inachukuliwa kuwa ni kama yeye ni mojawapo wa anayehusika katika shughuli za mahakama hivyo kuegemea upande mmoja ambapo hutoa msaada wa maoni yake.

Mazingira ya mahakama yanamshurutisha mtu kutumia lugha yenye urasmi mwingi hasa katika masuala ya vyeo na heshima. Utulivu na umakini kortini ni mambo ambayo huzingatiwa. Kwa sababu ya hali hizi mshtaki au mshtakiwa wanapotumia lugha isiyo na adabu wakati mwingine mfasiri huingilia kati swala hili kwa kumfanya mshtakiwa anayetoa ushahidi atulie

katika kesi. Katika kufanya hivyo mfasiri, hulegeza ukali katika maswali yanayoulizwa kwa kutumia maneno ya heshima au tafsida jambo hili linazua shida kwa sababu mfasiri kwa kuongeza yasiosemwa anakuwa ni kama mmoja wa wanaohusika katika kesi. Mfasiri hatekelezi wajibu wake badala yake anawasaidia wahusika.

Mamlaka na nguvu walio nao wanasheria pia inawawezesha kuuliza maswali kwa njia ambayo itakanganya mshtakiwa ili atoe majibu kwa njia fulani jambo linajitokeza wazi wakati hakimu atauliza swali au kiongozi wa mashtaka akitaka jambo fulani lifafanuliwe. Mikakati ya kuuliza maswali mafupi na pia yaliyo na ukali hutumiwa. Hii huathiri mfasiri ambaye hutakikana kuonekana hana heshima na pia ameuliza swali fupi lisiloeleweka. Mfasiri hurefusha swali au pia huongeza maneno yenye upole. Mfasiri huathiri mikakati ya kuuliza maswali ni kama yeye ni mmoja wa wahusika wa kesi.

Bente (2009) anasema nyongeza hutokea kulingana na jinsi mtindo wa ushahidi utakavyotolewa. Iwapo ushahidi ni wa masimulizi au unatolewa visehemu au vipande vipande, Pale ambapo mshtakiwa hajielezi vizuri mfasiri huchukua wajibu na kutoa masimulizi jinsi ameelewa kesi hiyo ili mfasiri aonekana ameimarika katika kazi yake. Athari ni kuwa habari au ujumbe ambao ulikuwa umeelezwa katika vipande vidogo unarefushwa na kuwa katika masimulizi hivyo kubadilisha yaliyosemwa. Hapa twapata kuwa mfasiri hubuni mambo yake au kufikiria yale ambayo hayakutolewa katika ushahidi.

Shida katika mawasiliano husababisha nyongeza katika ujumbe. Iwapo wahusika watakosa kuelewana, majibu ambayo yatakayotolewa hayataenda sambamba na maswali yaliyoulizwa. Hii ilisababishwa na tofauti katika utamaduni, tafsiri mbovu au kukosa kufuata ushahidi unaotolewa. Iwapo mfasiri alijua kuna shida hii alijaribu kuwaelekeza kwa njia fulani ili mawasiliano yasikatike. Mfasiri aliongeza ujumbe fulani ili mawasiliano yaendelee.

Makosa ya udondoshaji yalijitokeza pale ambapo sehemu zote zilizo katika LC hazikuzingatiwa katika LL. Chanzo chake ni wafasiri. Sababu ya makosa haya ni kutokana na ukosefu wa tajriba. Ukosefu wa elimu kabambe husababisha mfasiri kukosa istilahi mwafaka au kisawe mwafaka.

Makosa ya utamaduni yalitambuliwa. Ili kufasiri dhana za kitamaduni mfasiri anayetumia lugha za Kiingereza na Kiswahili huhitajika kupata visawe vya kitamaduni vilivyo mwafaka katika lugha anazozifanyia kazi. Visawe hivyo visipopatikana, basi mfasiri alipata matatizo makubwa. Isitoshe, makosa ya maana potovu na makosa anuwai yalitambuliwa.

Mambo yaliyochangia matatizo katika ukalimani yalijumuisha

i. Msamiati wa kitaaluma / sheria
ii. Maneno ya kawaida lakini yaliyo na maana tofauti
iii. Misemo- haiwezi ikatafsiriwa kutoka LC hadi LL
iv. Neno moja lakini iliyo na tofauti na maana katika LL
v. Sarufi – Vitenzi, vishazi, Kirai
vi. Nambari na majina- masaa, nambari, idadi, nafsi
vii. Sajili
viii. Mahali- neno lilipo mfano. Swali / mshangao katika sentensi.

5.2.2 Kubainisha kiini / chanzo mbalimbali ya matatizo ya tafsiri na ufasiri

Mtafiti alibainisha kuwa kuna chanzo mbalimbali ya matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama. Baadhi ya matatizo chanzo chake ni wanaofasiri. Hii ilijitokeza kwa kuwa kazi ya ukalimani haikupewa uzito unaostahili. Mtafiti alibaini kuwa kazi ya ukalimani ilichukuliwa inaweza fanywa na mtu yeyote kwa sababu wafasiri walikuwa ni wale ambao walikuwa wameajiriwa kama makarani na hivyo kufanya ukalimani ilipobidi. Isitoshe, ilichukuliwa kwamba kadiri unapoifanya kazi hii ndipo unakuwa na tajriba. Ingawa kwa kiasi kikubwa tajriba ni muhimu kwa sababu ya ujuzi wa muda mrefu iwapo mmoja alifanya kosa na bila kurekebishwa basi kuna uwezekano wa kuwa na matatizo mengi.

5.3 Hitimisho

Katika utafiti huu, tulitoa matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama. Madhumuni ya utafiti huu yalikuwa ni kutambua matatizo ya tafsiri na ufasiri na chanzo cha matatizo haya. Tulitambua kwamba, tafsri na ufasiri zilipofanywa kutoka LC hadi LL kulikuwa na matatizo ya ukosefu wa visawe mwafaka kwa sababu ya tofauti za utamaduni za lugha mbili tofauti, matatizo ya nyongeza, matatizo ya udondoshaji, matatizo ya maana potovu na matatizo anuwai. Matamko yaliyochanganuliwa yalithibitisha ukweli wa nadharia tete ya kwanza iliyodai kuwa, kuna matatizo ya tafsiri na ufasiri katika mahakama ya Kitale. Jedwali namba 16 linaakisi hali hii. Pia, matamko na mahojiano kutoka kwa wasailiwa yaliyochanganuliwa yamekubaliana na nadharia tete ya pili, iliyodai kuwa, kuna kiini / chanzo mbalimbali ya matatizo ya tafsiri na

ufasiri katika mahakama ya Kitale. Jedwali nambari 17 linathibitisha hali hii. Baadhi ya matatizo chanzo chake ni wanaofasiri.

Matokeo haya ya utafiti yaliafikiwa kupitia kwa nadharia ya Nida ya tafsiri iliyoongoza utafiti huu. Licha ya matatizo tutakayoelezea katika sehemu ya 5.4, ni muhimu kuelewa kwamba, madhumuni yetu ya utafiti yameafikiwa na nadharia tete zimethibitishwa kuwa sahihi.

5.3 Mchango wa utafiti

Utafiti huu ni muhimu kwa wasomi hasa katika taaluma ya isimu kwani imechangia katika tafsiri na ufasiri. Mchango huu ni muhimu katika kupanua mawazo kuhusu tafsiri na ufasiri kwa kuchunguza matatizo yanayoweza kukatiza mawasilano na kukabiliana nayo.

Isitoshe, utafiti huu unachangia katika uchanganuzi semi na hasa katika nyanja pana ya sajili ya mahakama.

5.4 Matatizo yaliyomkabili Mtafiti

Ilikuwa vigumu kupata vitabu vilivyohitajika katika utafiti huu. Vitabu vilivyopatikana ni vilivyoandikwa kwa lugha ya Kiingereza. Hii ililazimu tafsiri ifanywe kama sharti la kazi hii. Baadhi ya dhana tulizozipata zilikosa visawe vyao katika lugha ya Kiswahili. Hii ilitufanya kuwa na maelezo ambayo huenda yasiibue maana iliyokusudiwa katika muktadha asilia. Hata hivyo, mtafiti alijaribu kuleta uwiano kati ya lugha chanzi na lengwa. Kwa upande mwingine, mtafiti aliweza kukumbana na masuala mengine nyeti ya taaluma ya uanasheria kwa sababu hajasomea uanasheria hata ingawa alipata msaada kutoka kwa mawakili. Hii ilikuwa ni changamoto.

5.5 Mapendekezo

1) Utafiti ulionyesha kuwa kulikuwa na haja ya mawakili kuwa katika mstari wa mbele katika kumkumbusha kila mara mfasiri wajibu wake katika kazi ya ufasiri. Pale ambapo mfasiri haelewi wajibu wake hakimu awe tayari kumwelekeza. Mkalimani akumbushwe kuwa wajibu wake ni kufanikisha mawasiliano kati ya mshtakiwa, mshtaki, wakili pamoja na jaji au hakimu. Ni muhimu mkalimani afahamishwe kuwa ahitajiki kutoa mawaidha ya kisheria wala si kujibu maswali au kusaidia yeyote. Mikakati mingine ni kuhakikisha kuwa maswali yote yanaulizwa kupitia hakimu. Mfasiri hahitaji kujibu maswali bali kufasiri jinsi yanavyoulizwa. Iwapo kutatokea shida katika mawasiliano mfasiri afahamishe jaji au wanaohusika.

2) Hakimu pia ahakikishe kuwa kuna utulivu katika kortini hasa pale ambapo kuna kukatizana kauli. Ni wajibu wake kuhakikisha kuwa mhusika mmoja anaongea kwa wakati wake. Wakalimani wasitumie nafsi ya kwanza "mimi" ili isilete utata. Mkalimani amrejelee mshtakiwa au mshtaki. Hakimu ahakikishe kuwa wahusika wanaongea kwa sauti inayosikika ili mawasiliano yasikatike. Iwapo mmoja ataongea kwa muda mrefu ishara zaweza kutumika kuashiria atulie au ampe mwingine nafasi pia aseme. Ilibainika kuwa kulikuwa na haja ya kuwapa wafasiri fursa ya kurekebisha makosa pindi yanapotokea ili yasipotoshe. Hakimu aliwajibika kuwakumbusha washtakiwa kuwa kazi ya mkalimani si kuwasaidia kufafanua zaidi yanayojiri mahakama bali kufanikisha mawasiliano. Pia, wahusika washauriwe kuwa hata kama wanaelewa lugha zote mbili za ukalimani unaofanywa ni vyema wangojee swali katika lugha iliyokuwa ikitafsiriwa. Majibu yote yaelekezwe kwa jaji bali si mfasiri.

3) Wasailiwa walipendekeza kuwa kulikuwa na haja ya kuzingatia ufasiri bora katika mahakama kwa sababu ya umuhimu mkubwa unaotekeleza. Kuna haja ya wafasiri wazingatie ufasaha wa lugha, bali na kujua lugha husika itabidi kuelewa utamaduni wa wanaohusika katika lugha hizo. Walipendekeza kuwa ni bora kuzingatia maadili na sheria ambazo ni muhimu katika tafsiri. Kulikuwa na haja ya kuzingatia uaminifu wa kiapo wanaochukua kabla hawajaanza kazi hii ya ukalimani.

4) Kama ilivyo katika nchi ambazo zimepiga hatua katika ukalimani kama vile Australia au Uholanzi kuna haja ya kuiga yanayoendelea kule kwa mfano, kwa kuwa na viapo vya wafasiri mahakama itakayoongoza taaluma hii katika mahakama kwa kutoa maadili, vigezo na masharti maalum katika kutekeleza na kuona kwamba wanaofanya kazi hii ni wale waliofuzu tu.

5) Kuna haja ya kuwapa mafunzo wafasiri. Kozi zaweza kuwa za muda mfupi au muda mrefu. Kozi za muda mfupi ziwe za gharama ya chini, zaweza kuwa warsha ambazo zitatilia maanani taaluma ya ukalimani au mambo muhimu ambayo yanaweza zingatiwa hasa kuhusu wajibu wa mkalimani. Kozi za muda mrefu ziwe na urasmi wa utaratibu wa masomo yalio na nia ya kuinua stadi za ukalimani, kuinua kiwango cha lugha mbili husika na stadi za ukalimani zitakazotumia mikakati mwafaka kwa lengo ya kuimarisha au kuboresha ukalimani, kujua lugha vyema pamoja na kusoma na kunena lugha hizi katika hali ya mazoea kwa kufanya mazoezi.

Ili kuwa na wakalimani ambao wamefuzu ni lazima:

i. Kutoa mafunzo kabambe kuhusu ukalimani kortini.

ii. Kuchapisha makala itakayosaidia masuala ya mahakama na sheria.

iii. Kuwaelimisha wakalimani wanaofanya kazi jinsi ya kuboresha kiwango cha lugha na kuwasaidia kujenga vipawa vyao vya kazi yao.

6) Kuna haja ya kuzungumza na kujua lugha husika zitakazotumika katika ukalimani na pia kusoma na kuongea lugha hizi. Jambo hili litaongeza ujuzi katika kupanua uelewa wa ukalimani. Katika kufanya hivi, itaongeza idadi ya wafasiri waliofuzu katika ukalimani.

7) Isitoshe, mahakama itafanikisha ukalimani kwa kuchapisha na kutoa makala ya kusomwa kwa wafasiri itakayokimu mahitaji yao. Makala haya yashughulikia mada kama sheria au sajili ya sheria itakayopanua viwango katika msamiati, wajibu wa mkalimani ajue mambo anayotarajia kupata katika mahakama, hospitali, mahakama ya watoto.

Suluhisho ya chanzo cha matatizo:

i. Ukosefu wa elimu na ujuzi kabambe ushughulikiwe.
ii. Kutambua na kurekebisha makosa yanayofanywa.
iii. Kuwa mvumilivu na mwaminifu katika hali tunazokumbana nazo.
iv. Wahusika wajulishwe wajibu wa mkalimani.

5.6 Utafiti zaidi

Kuna haja ya kufanya utafiti zaidi katika ukalimani na ufasiri kwa kina nchini Kenya. Tafiti zifuatazo zingeshughulikiwa ili kutoa mwelekeo utakaodhihirisha:

i. Kuchanganua uamuzi wa jaji katika kesi ambapo tafsiri na ufasiri umefanywa.
ii. Kuchanganua ripoti za Polisi ambazo huandikwa kwa Kiingereza hata ingawa zitakuwa zimeelezwa kwa lugha tofauti na Kiingereza.
iii. Kuna haja ya kuchunguza ujumbe katika vitabu ambavyo vimetafsiriwa kutoka lugha nyingine hadi Kiswahili.

MAREJELEO

Bazerman, C. (1981). "What Written Knowledge Does: Three examples of Academic Discourse." *In philosophy of the social sciences pp,* 361-387.

_____ (1992). "Bilingual Court Proceedings: The Role of the Court Interpreter" in Judith, N.L (ed.) *Language in the Judicial Process*. Plenum Press.

Bell, R.T. (1991). *Translation and Translating Theory and Practice*. London: Longman Group UK Limited.

Bente, J (2009) "Additions in Court Interpretation. A PHD project Investigating the Language of court Interpreters in the Danish Courtrooms" . Haijachapishwa. http://www.criticallink.org/files/cl2.Jacobedenpdf accessed 11th Aug 2011

Best, J.W & Khan, J.V. (2003). *Research in Education* (2nd Ed). New Delhi: Asoke K. Ghash

Bolinger, D (1980). *Language the Loaded Weapon.* Bloomington, Indiana: Indiana University Club

Brazil, D. (1995). *A Grammar of Speech*. Oxford: Oxford University Press.

Bri'ere, E (1978). "*Limited English Speakers and the Miranda Rights* Katika: Tesol Quartely 12 (3) pg 234-45

Brower, A.R. (1966). *On Translation*. New York: Oxford University Press.

Brown, G. (1995). *Speakers, Listeners and Communication: Explorations in Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.

Brown, G. & Yule, G. (1983). *Discourse Analysis*. Cambridge: Cambridge University Press.

Bryman, A. (2001). *Social Research Methods*. New York: Oxford University Press.

Cotterill, J. (2002). *Language in the Legal process*. London: Palgrave Macmillan Ltd.

Coulthard, M. (1985). *An Introduction to Discourse Analysis.* London: Longman Group Ltd.

Cremona, V. & Mallia, H. (2004). *Language and Diplomacy Interpretation*.Malta:Diplo Projects.

Danet, B. (1980). "Language in the legal process" in Law and Society, Review 14: 445-564

De Jongh, E.M. (1992). *An Introduction to Court Interpretating: Theory and Practise*.New York: University Press of America.

Golingay, J. (1995). *Models of Interpretation of Scriptures*. Michigan: William B. Eerdmans Publishing Company.

González & Vásquez & Mikkelson (1991). *Fundamentals of Court Interpretation: Theory and Practice*. Durham; North Carolina: Carolina Academic Press.

Grice, H.P. (1975). 'Logic and Conversations ', in P.Cole and J. Morgan (eds), *Syntax and Semantics 3: Speech Acts*. Newyork: Academic Press, pp.41-58.

Hale, S.B (2004). *The Discourse of Court Interpreting*. http://www.nesconline.org/wc/publications accessed 23/11/2011 .

Hughes, A. (1989). *Testing For Language Teachers-Cambridge*: Cambridge University Press.

Human rights watch. (2010). "*All the men have gone*" http://www.human rights watch.htm Accessed on 5/11/2010.

Kaschula, R.H. (1995). 'Cross-Cultural Communication in the Eastern Cape with particular reference to Law Courts', *South African Journal of African Languages*, Vol.15 (1), pg.9-15.

Kioga, M.M. (1992). "Administration of Justice in the Rural Areas of Kenya" *in Law and Society*. Nairobi: The international Commission of Jurists (pp.74-82).

Kombo, D & Tromp, D. (2006). *Proposal and Thesis Writing: An Introduction*. Nairobi: Paulines Publications.

Kothari, C.R. (2003). *Research Methodology -Methods and Technigues.* New Delhi: Washwa Prakashan.

Leech, G. & Svartik, J. (2002). *A communicative Grammar of English.* London: Pearson Education Ltd.

Leech, G.N. (1995). *Principles of Pragmatics* . New York: Long man Group Ltd.

Lovejoy, B. (1991). "Cohesion and Information Strategy in Academic Writing: Analysis of Passage in Three Disciplines." *In Linguistics and Education,* pp.97-112.

Mazrui, A. M. & Ali, A. (1998). *The Power of Babel. Language & Governance in the Africa Experience.* Nairobi: East African Educational Publishers.

Merriam, S. (1998*). Qualitative Research and Case Study Application in Education.* San Francisco: Bass Publishers.

Mills, S. (1999). *Discourse.* London: Routeledge.

Milroy, J. (1984). "*Sociologistics Methodology and the Identification of speakers*" Voices in Legal Proceedings: Katika Trudgil (1984 a) pg 51-72

Milroy, J. (1987). *Observing and Analyzing Natural Language*. Oxford: Basil Blackwell.

Mikkelson, H. (1998). *Towards a Redefination of the Role Court Interpreter.* http://www.acebo.com/papers/guarantr.htm accessed 25th May 2009.

Moeketsi, R. (1999). *Discourse in the Multilingual and Multicultural Courtroom: A Court Interpreters' Guide.* Pretoria: Van Schaik Publishers.

Moeketsi, R.H. & Swanepoel, C. F. (1997). *Souther Sotho: Only Study Guide SSE 302-5.* Pretoria. University of South Africa.

Musau, P. (2003). "*Linguistic Human Rights in Africa: challenges and Prospects for indigenous Language in Kenya"* Language, culture and Curricullum, Vol.16, no.2. http://www.multilingualmatters.net/icc/016/icco160155 accessed 18th June 2010.

Mutunga W. (1990). *The Rights of an Arrested and an Accused Person.* Nairobi: Oxford University Press.

Mugenda, O.M. & Mugenda, A.G. (2003). *Research Methods: Quantitative Approaches.* Nairobi: Acts Press.

Mutai, B. (2000). *How to Write a Quality Research Proposal. A complete & Simplified Recipe.* New Delhi: Thelley Publications.

Mwansoko, H. J. (1996). *Kitangulizi cha Tafsiri.* Dar es Salaam: TUKI.

Newmark, P. (1988). *A Textbook of Translation.* London: Prentice Hall International..

Nida E.A. (1964). *Towards a Science of Translating.* Newyork: Leiden, Brill.

_____ (1969). *The Theory and Practise of Translating.* Newyork: United Bible Societies.

Ogechi, N. & Shitemi, N. & Simala, K. (2008). *Nadharia katika taaluma ya Kiswahili na lugha za Kiafrika.* Eldoret: Moi University Press.

Ogula, A.P. (2003). *Research Methods.* Department of Education. The Catholic University of Eastern Africa

Okeiga, N.I (1998). "Sajili ya Kisheria katika Mahakama za Kenya: Vizuizi, Athari na visaidizi katika matumizi zaidi ya Kiswahili". Haijachapishwa.Tasnifu ya uzamili Chuo Kikuu Cha
Moi.

Orodho ,A.J. (2004). *Techniques of Writing Research Proposals & Reports in Education & Social Sciences.* Nairobi: Masola Publishers.

Owala, S.O. (2006). "Matatizo Kwenye Ujumbe Katika Kalimani ya Kidini Mjini Bondo." Haijachapishwa.Tasnifu ya M.A Chuo Kikuu Cha Egerton.

Palmer, C. B. (1996). *Towards a Theory of Cultural Linguistics.* Austin: University of Texas Press.

Roy, C. (2000). *Interpretating as a Discourse Process.* Oxford: Oxford University Press.

Saville –Troike, M. (1989). *The Ethnography of communication an Introduction.* London: Basil Blackwell.

Schiffrin, D. (1995). *Approaches to Discourse* O.U.P: Blackwell Publishers Inc

Seal, C. (2004). *Researching Society and Culture.* New Delhi: Sage Publishers.

Seligson, S.B. (1990). The Bilingual Courtroom: *Court Interpreters in the Judicial Process. Chicago*: University of Chicago Press.

Shitemi, L. (2010). *Ushairi wa Kiswahili Kabla ya Karne ishirini.* Eldoret: Moi University Press.

Shlesinger, M. (1991). 'Interpreter Latitude vs. Due Process.Simultaneous and Consecutive Interpreting in Multi-Lingual Trials', in S.Tirkonnen-Condit (ed.) *Empirical Research in Translation and Intercultural Studies.*Tubingen: Gunther Narr Verlag, pg.147-55.

Silverman, D. (2005). *Doing Qualitative Research.* London: Sage Publications.

Sure, (1991). "Language Functions and Language Attitudes: Acase of Diglossia in Kenya" Paper presented at English conference, Nairobi March 1986.

Taft, R. (1981). "The Role and Personality of the Mediator", in S. Bochner (ed), *The Mediating Person*: Bridges Between Cultures. Cambridge: Schenkman, pg.53-88.

Thomas, J. (1995). *Meaning in Interaction*: *An Introduction to Pragmatics*. London: Longman

Tudor, J. (1988). *The law of Kenya.* Nairobi: Kenya Literature Bureau.

Walker, A. (1982). "Patterns and Implications of Co- Speech in a Legal Setting" katika Di Pietro Pg 101-12

Wadensjö, C. (1998). *Interpreting as Interaction.* Harlow: Addison Wesley Longman.

KIAMBATISHO A

Dodoso kwa wafasiri / wakalimani

Dodoso hii imekusudiwa kukusanya habari kuhusiana na maoni kuhusu ukalimani. Habari zote utakazotoa zitahifadhiwa kwa siri na mtafiti na kutumika kufikia malengo ya utafiti huu. Ushirikiano na uaminifu wako katika kutoa habari sahihi utathaminiwa sana.

Sehemu ya A: Taarifa za kimsingi

Jinsia

a) Mke
b) Mume

Umri

a) Chini ya miaka 20
b) Miaka 20-25
c) Miaka 26-30
d) Miaka 31-35
e) Miaka 36-40
f) Zaidi ya miaka 41

Elimu

a) Uzamili
b) chuo kikuu
c) Kidato cha sita
d) Kidato cha nne
e) Nyingine yoyote

Tajriba katika ukalimani

a) Chini ya mwaka 1
b) Mwaka 1-3
c) Mwaka 4-6
d) Mwaka 7-10

e) Zaidi ya miaka 10

Sehemu ya B

1. Umeenda kozi gani za ukalimani?

   a) Chuo kikuu
   b) Diploma
   c) Cheti cha shahada katika ukalimani
   d) Warsha / semina / Kongamano
   e) Nyingine

2. Je, kuna haja ya wakalimani kupewa mafunzo ya sheria na mbinu mwafaka za ukalimani? Eleza

3. Ni nini jukumu au wajibu wako kama mkalimani?

4. Ni matayarisho gani wewe hufanya kabla ya kufanya ukalimani?

5. Kuna wakati ambapo washtaki / washtakiwa hulalamika kuwa kile ukalimani sicho walichosema au kusudia? Eleza

6. Ni changamoto gani wewe hukumbana nazo katika kazi hii ya ukalimani?

7. Kwa maoni yako wewe, hukabiliana vipi unapokumbwa na matatizo yafuatayo.

   a) Ukosefu wa visawe mwafaka
   b) Tofauti za utamaduni na mazingira
   c) Tofauti katika maumbo ya lugha mbili
   d) Kutoelewa sehemu fulani

8. Toa tafsiri ya maneno haya kama unavyoyatumia katika shughuli yako ya ukalimani.

   a) Mitigation

b) Defense
c) Carnal knowledge
d) Plea
e) Burglary and Housebreaking
f) Jurisdiction
g) Cross-examination
h) Robbery with violence
i) Confessions
j) Indecent assault

9. Pendekeza jinsi ukalimani unavyoweza kuboreshwa.

KIAMBATISHO B

Dodoso kwa hadhira

1. Kwa maoni yako ufasiri umefanywa vipi?

    a) Vizuri

    b) Wastani

    c) Haukueleweka

    d) Haukuwa wa haki

2. Je, maamuzi ambayo yametolewa na hakimu yalienda sambamba na yaliyotafsirwa?

3. Je, kuna sehemu ambazo unafikiria hazikufasirwa vizuri? Eleza

4. Je, kuna sehemu zilizofasiriwa ambazo haukuzielewa. Kwa nini?

5. Toa maoni yako njia ambazo zinaweza kuboresha ufasiri katika mahakama.

KIAMBATISHO C

MATAMKO

Ufafanuzi wa alama

...	-	Inaonyesha kuna maneno yalioachwa au msemaji anatulia au kufikiria au baada ya muda au matumizi ya viziada lugha.
C3.1	-	inaonyesha matamko ya kikao 3 mstari wa 1
( )	-	Tafsiri iliyofanyika ili upande wote uelewe.
Wino mzito(Italiki)	-	umetumika kuonyesha sehemu zilizozingatiwa katika uchanganuzi.

PR-Prosecutor / kiongozi wa mashtaka

MA-Magistrate/ hakimu

AC-Accused /mshtakiwa

CO- Complainant/mshtaki

IN-Interpreter/ mkalimani

WI-Witness/ shahidi

C 1

2/3/2011 saa 9:04 asubuhi
Criminal case No. 793 of 2010
R –v- Benson Kiptarus Ndiwa

(Mshtakiwa alikuwa ameshtakiwa kwa wizi wa Ng'ombe)

1. **PR:** Your honour, in this matter I wish to apply for an adjournment. My next witness who is ***the investigating officer, is not feeling well...***

2. **MA:** Yes, when is he expected back?

(Baada ya mashauriano dakika 3)

3. **PR: I *have been informed he will be back in 3 days time, your honor.***

4. **MA:** Yes, any ***objection?***

5. **IN:** Kiongozi wa mashtaka anaomba kesi ihairishwe kwa sababu yule shahidi alikuwa aitetee hayuko. ***Unakubali au unapinga?***

(...Baada ya kimya kirefu)

6. **AC:** ***Sielewi.***

7. **IN:** ***Unakubali au unapinga***? Hilo ndilo swali .
8. **AC: ... (anatikisa kichwa)**

(kesi hii itasikizwa tarehe 9 Machi)

C2

3/3/2011 saa 10:55 Asubuhi
Criminal case No. 2702 of 2007
R –v- Daniel Mwangi Munyoro Githinji
(Kesi ilikuwa inaendelea mashahidi walikuwa wakitoa ushahidi. Kesi ilihusu mauaji)

1. **MA:** *Just a minute, who are the witnesses in this case?*

2. **PR:** *There are three more, your honour... the two girls, the complainants, the doctor and the investigating officer... They are four, your honour.*

3. **MA:** *Have you checked on P3 forms...the doctor's conclusion?*

4. **PR:** *Your honour. I have not had time to....*

5. **MA:** *Isn"t that not a file.*
6. **PR:** Y es...

7. **MA:** *This is an old matter, what does it say? any evidence brought before it'...*

8. **PR:** Yes. *Your honour.*

9. **MA:** *Will doctor's evidence and the investigating officer help us...*

10. **PR:** *Yes, it seems ...but we need more clarification..may be girls..*

11. **MA:** *How old are the girls... the victims?*

12. **PR:** *They are — both of them are 8 years old, your honour.*

13. **MA:** *Are there no adult witness, a person who may have seen the accused with the girls? You know ... because the only real evidence you have is what the girls will say. There is no way the court will convict somebody on the basis of the testimony of eight-year olds about something that happened over two month ago. Do you get what I am saying? This won't work.*

14. **PR:** *Yes. Your honour, I think I will link with*

    the investigating officer to find out if there are other witnesses so that...

15. **MA:** *You will know what to do for now. Let's take a hearing date. Eh...9th March?*

16. **PR:** *Most obliged your honour.*
17. **IN:** *kesi yako itasikizwa tarehe 9 machi*
    (Your case will be heard on 9th March.)

C3

7/3/2011 saa 4:23 jioni
Criminal case No. 449 of 2011
R –v- Linda N. Wekesa

(Kulikuwa na wizi wa vitu)

1. **CO**: If I tell the court you ***were beaten up because you had developed a habit of Visiting me when my husband is not there, would I be lying?***

2. **IN**: Nikieleza mahakama kuwa ulikuwa umezoea kuja kwangu usiku kila siku ukijua mume wangu ***hayuko nitakuwa nikidanganya?***

3. **AC:** ***Stop that madness. Are you insane? do you want to say that Iam the one who broke into the house and stole the T.v ?***

4. **IN:** ***You...do you realize you are in court****, you...*

5. **MA**: What is his answer?

6. **AC**: ***Those are lies, your honour.***
7. **IN:** ***Eleza mambo yanayohusiana na wizi wa televisheni...***

(kesi imehairishwa mpaka tarehe 23/3/2011)

C4

9/3/2011 9:30 Asubuhi
Criminal case No. 68 of 2010
R -v- Daniel Chege Njoroge

(Kesi hii ilikuwa inaendelea na ushahidi ulikuwa unatolewa. Ilihusu ubakaji)

1. **WI:** ***on observation, the patient's vagina and vulva were swollen and bruised.The hymen was also broken. This was enough evidence that somebody had had carnal knowledge of her that involved actual penetration.***

2. **IN**: Daktari alipomkagua alipata ushahidi kuwa ***ulimfanyia kitendo hicho***. (When the doctor examined her, he found evidence that you had done that act on her.)

3. **AC:** No your honour, I did not ***touch her I just touched the upper part and the lower part***

4. **IN:** ***Alimgusa sehemu ya juu tu na chini tu***.

5. **MA:** what exactly do you mean by ***upper part and lower part***?

6. **AC:** The breasts and the pants

7. **IN:** Matiti na nguo ndogo.

8. **MA**: Did you have ***carnal knowledge*** of the complainant?

9. **IN**: Je ***ulimnajisi mshukiwa*****? (did you rape her?)**

10. **AC:** No, we agreed and she gave me.

11. **CO:** La sikukubali aliniambia ***nimsave nimpe huku chini***" jambo nililokataa

12. **PR:** Yes your honour, I think I will link with the investigating officer to find out if there are other witnesses so that...

13. **MA:** Let's take a hearing date. Eh...16th March?

14. **PR:** Most obliged your honour.

15. **IN: kesi yako itasikizwa tarehe 16 machi**

C5

16/3/2011 saa 11:45 Asubuhi
Criminal case No. 1835 of 2010
R –v- Moses Hassan Oli

(Kesi ilikuwa imeanza mwaka 2010 mshtakiwa alipatikana na misokoto ya bangi)

1. **PR:** Considering the evidence on record. Iam convinced that the prosecution has proved its case beyond any reasonable doubt and the accused person is quilty as charged.

2. **MA**: ***Mitigation?***

3. **IN:** ***Malilio.***
4. **AC:** Eh....

5. **IN:** ***Kuna kitu ungetaka kuambia*** mahakama kabla huja hukumiwa?

   (Is there something you would like to tell the court before you are sentenced?

6. **AC**: Ndiyo. Ningetaka kuambia korti mimi nikuwekelewa nawekelewa haya mambo.

   Polisi Walinipata usiku nikienda kwangu na wakataka ***kitu kidogo*** kwangu na sikuwa nacho na hivyo ***wakaniweka hii*** kitu mfukoni.

   (Yes, I would like to tell the court these are false allegations being made against me. The Police found me at night and wanted some money which I didn't have and so they planted on me some bhang)

7. **IN:** ***Hii sio saa za kuelezea vile ilikuwa. Si ulitoa ushahidi wako? Umepatikana***

   na hatia na sasa inatakikana useme kama una shida yoyote korti inaweza kuangalia kabla haujahukumiwa.

   (This is not the time to explain the way it was. Didn't you give your testimony? You have been found guilty and now you are required to say whether you have any problems that the court can consider before sentencing you…)
   Uko na watoto? (Do you have children?)

8. **AC**: Ndio. (Yes.)

9. **IN:** ***Eeh … useme vitu kama hizo ... watoto... bibi … kama uko na ugonjwa fulani, wanaokutegemea.***
   (Yeah … say things like those … children … a wife ... whether you have a certain illness …dependants... your job security.

10. AC: Nina shida nyingi unisamehe

(Kikao kimehairishwa mpaka saa nane wakati uamuzi utatolewa)

(Baada ya chakula cha mchana)

11. MA: Following the evidence and subsequent cross –examination it has been proved that you were found in possession of bhang against our laws and therefore you are sentenced to seven years so that it may be a lesson to you and others. Any appeals to be done before 14 days.

12. IN: ***Umehukumiwa miaka saba. Umepewa siku 14 kukata rufaa.***

C6

24/3/2011 saa 4:04 Jioni
Criminal case No 443 of 2011
William Adera Goga

(Kesi hii ilihusu vita. Kesi hii ilikuwa imetajwa mara kadha na ilikuwa inaendelea)

1. **AC**: ***I beat him with 3 blows of hammer***

2. **IN:** ***Alimpiga na nyundo tatu.***

3. **CO:** Nilihustle naye mpaka nikabaki na nyundo ambayo nataka kuitoa kama Ushahidi. (I managed to struggle with him till I retained the hammer and I intend to use it as exhibit).
4. **PR:** where are the hammers?

5. **IN**: Wapi nyundo?

6. **CO:** Kwani husikii nimeitoa kama ***exhibit.***

7. **AC**: Your honour, I totally disagree because I had only one hammer I don't know of the two others.

8. **IN:** ***sikubali mashtaka kwani nilimpiga nyundo tatu***

9. **MA:** Lets take another hearing date…16th

10. **IN:** ***Kesi hii imehairishwa kwa sababu ya ushahidi ambao si kamili.***

C7

6/4/ 2011 saa 3:12 Jioni
Traffic case No. 861 of 2010
R –V- Joseph Wachira

(Kesi inahusu ajali ya barabara)

1. **CO:** Mheshimiwa aliponigonga aliendesha gari ovyoovyo najua huwa analewa.
2. **AC:** I would like to tell this court that ***I have never driven when I'm drunk***.
3. **IN**: Anasema kuwa hajawahi lewa garini.
4. **CO:** Lakini si wewe ***huchapa maji***?
5. **MA**: Yes... ask questions that will help the court.
6. **IN:** Uliza maswali yatakayokusaidia.
7. **CO:** ***Kwani nafanya nini?***
8. **IN:** Heshimu korti eleza ushahidi mwingine.
9. **AC:** How did you know that I was driving reckless when there was jam***?***
10. **IN:** Ulijuaje niliendesha gari vibaya na kulikuwa na jam?
11. **CO:** Watu walikuona na wewe huendeshaga hivyo.
12. **MA**: Can you bring those people to bear testimony?
13. **IN:** ***Una mashahidi?***
14. **CO:** Ndiyo lakini hawako hapa lakini hata kila mtu anajua kuwa alinigonga.
15. **MA: The case will be heard on May, 28th.**
16. **IN**: Kesi itasikizwa Mei, 28 uje na ***mashahidi.***

C8

14/4/2011 saa 9:32 asubuhi
Criminal case No. 917 of 2011
R –v- Joseph Oteba Papa

(Mshtakiwa alieleza jina lake, anakoishi, kazi anayofanya na kisha alisomewa mashtaka; alipatikana na silaha kinyume na sheria)

1. **MA:** You are charged with possession of A.K 47 gun with 5 rounds of ammunition. Do you plead guilty or not?

2. **IN:** ***unakubali mashtaka au unakataa?***

3. **AC:** ***Nakataa.***

4. **MA:** You have been given a bond of five hundred thousand shillings or something of equal Value to that money.)

5. **IN:** Utoe ***bondi*** ya shilingi elfu mia tano au thamani ya kitu kinachotoshana na pesa hizo.

6. **AC:** ***Kitu kama ...?***

7. **IN :** Kitu kama cheti cha kumiliki shamba hata kama ni ya jamii yenu

8. **ACCUSED:** Ndio watu wa jamii wako hapa.
   [Akielekeze kidole kwa aliye simama)

9. **MA:** [Addressing the person who has stood up]

   (If it is a title deed you want to bring, you take it first for a valuation to be done, that piece of land to be seen is of what value. The letter you will be given when the valuation is done you come with it together with the title deed . Do you understand?)

10. **IN:** Nadhani umeelewa ***enda ulete barua***
    (... kesi itaendelea tarehe 28/ 4/ 2011)

EGERTON UNIVERSITY LIBRARY

C9

26/4/2011 saa 11:24 asubuhi
Criminal case No. 2590 of 2010
R –v- Job Barasa

(Kesi ilikuwa ya shamba kesi ilikuwa imetajwa hapo awali)

1. **PR:** Leo ikiwa ni siku ya kusikiza kesi yako unashtakiwa kwa kuuza shamba ya ekari 10 kwa wanunuzi wawili Kwa wakati mmoja...

2. **MA**: ***Defense.***

3. **IN:** Sasa ni wakati wako wa kujitetea.

   (Now is your time to defend yourself).

   Na kuna njia tatu za kujitetea. Unaweza kujitetea ukiwa hapo ambapo upo hautaapishwa na hautaulizwa maswali na korti au kiongozi wa mashtaka na Kama uko na mashahidi unaweza kuwaita.

   (You can defend yourself from there [the dock], in which case you will not be sworn and you will not be asked questions by the court or prosecutor and if you have witnesses, you can call them.)

   Njia ya pili unaweza kuja upande huu ambapo utaapishwa na utauulizwa maswali na korti au kiongozi wa mashtaka na Kama na uko na mashahidi unaweza kuwaita.

   (The second way: you can come to this side [the witness stand], where you will be sworn and you will be asked questions by the court and the prosecutor and if you have witnesses, you can call them).

   Njia ya tatu na ya mwisho, unaweza kuamua kukaa kimya na uongenjee uamuzi wa mahakama.

   (The third way and the last one, you can choose to remain silent and await the decision of the court.)

4. **AC:** Sasa ipi ni nzuri. ***Sina mashahidi*** ...

(Kesi itaendelea)